VISION 2050

SEPTEMBA 28, 2026 /islamicftz

Rabi ul-Thani 17 1448

IMAAN

Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

ISSN 5618 - NO. 603



Magereza, The Islamic Foundation kuzidi kushirikiana kurekebisha wafungwa

Aref Nahdi: Amani iwe ajenda ya kudumu kwa maimamu

Serikali yazidi kujipanga kukabili athari za El niño

AMYC yaweka mkazo elimu inayoambatana na malezi ya kitabia

Mudir wa taasisi ya Ansar Muslim Youth Center (AMYC), Sheikh Salim Barahiyan

Dkt. Kassim ajenga hoja kuanzishwe Waqf wa kuzuia majanga nchini

Robo familia za Gaza zinaongozwa na wanawake

■ Takribani kaya 86,290 Gaza zinaongozwa na wanawake, karibu mara mbili ya kabla ya Oktoba 2023, wengi wakiwa wajane au waume zao wamepotea, wamezuiliwa, kujeruhiwa au kutoweka.

Dubai kumuomboleza Sheikh Ahmed Al Maktoum siku 10

MIMBARI ZETU

Ujumbe wa Imam Al-Dosari, Imam Al-Budair, Sheikh Ibrahim Twaha na Sheikh Hashim George kwa umma

إِنَّا لِلَّٰهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ

Dubai kumuomboleza Sheikh Ahmed Al Maktoum siku 10

Dubai inaendelea na siku 10 za maombolezo kufuatia kifo cha Sheikh Ahmed bin Rashid Al Maktoum, mdogo wa Mtawala wa Dubai Sheikh Mohammed bin Rashid Al Maktoum, aliyefariki Septemba 21, 2026 akiwa na miaka 76.

Wakati wa maombolezo, bendera zimeshushwa nusu mlingoti, huku viongozi kutoka ndani na nje ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) wakitoa salamu za rambirambi.

Rais wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan pia alitoa pole kwa Sheikh Mohammed, familia ya kifalme ya Al Maktoum, Serikali na wananchi wa UAE kufuatia kifo hicho.

Sheikh Ahmed anakumbukwa kwa mchango wake wa muda mrefu katika ulinzi, usalama, huduma za umma, uwekezaji na hisani, huku pia akiwa na historia kubwa katika michezo na mbio za farasi.

Alisomea masuala ya kijeshi katika Chuo cha Kijeshi cha Kifalme cha Sandhurst nchini Uingereza. Baada ya kuhitimu alijiunga na Central Military Command Dubai na baadaye kuwa kamanda wake.

Aliendelea kuhudumu kama Naibu Mwenyekiti wa Polisi ya Dubai na Usalama wa Umma, mojawapo ya nyadhifa muhimu katika mfumo wa ulinzi na usalama wa Dubai.

Mbali na majukumu ya serikali, alikuwa Mwenyekiti wa ARM Holding, kampuni binafsi ya uwekezaji ya UAE.

Alama katika hisani

Mchango wa Sheikh Ahmed haukuishia katika utumishi wa umma. Mwaka 2021 alitoa msaada katika uanzishaji wa Hamdan Bin Rashid Cancer Charity Hospital, hospitali ya hisani iliyokusudiwa kutoa huduma za saratani kwa wagonjwa wenye uhitaji.

Al Jalila Foundation ilimtaja Sheikh Ahmed miongoni mwa waliounga mkono hospitali hiyo, ambayo ilianzishwa kama hospitali ya kwanza ya hisani ya saratani nchini UAE.

Baada ya kifo chake, zimejitokeza pia simulizi za watu waliomfahamu zikieleza misaada aliyokuwa akiitoa bila kuitangaza.

Khaleej Times imeripoti ushuhuda wa raia mmoja wa UAE aliyesema Sheikh Ahmed aliwahi kugharamia matibabu ya mtu mwenye uhitaji na kuendelea kumsaidia mtoto wa mfanyakazi aliyefariki kwa takribani miaka 15.

NA MRISHO TOZO

Aref Nahdi ataka amani, umoja ziwe ajenda za kudumu kwa maimamu

■ Mwenyekiti Nahdi alielezea na kufafanua umuhimu wa viongozi hao wa dini kutumia uwezo na ushawishi wao katika jamii, kuwaelimisha Waumini kuhusu wajibu na faida ya kulinda amani na utulivu wa nchi.

TAASISI ya The Islamic Foundation imewataka Maimamu nchini kuendelea kuhubiri amani, umoja na utulivu katika jamii, ikisisitiza kuwa hiyo ni misingi muhimu ya ustawi wa watu na maendeleo ya Taifa.

Wito huo umetolewa na Mwenyekiti wa taasisi ya The Islamic Foundation, Aref Nahdi, wakati akizungumza katika semina iliyowakutanisha maimamu.

Kwa msisitizo mkubwa, Mwenyekiti Nahdi alielezea na kufafanua umuhimu wa viongozi hao wa dini kutumia uwezo na ushawishi wao katika jamii, kuwaelimisha Waumini kuhusu wajibu na faida ya kulinda amani na utulivu wa nchi.

Nahdi alisema Maimamu wana nafasi kubwa ya kuwaelimisha Waumini kuhusu umuhimu wa kulinda amani na kuepuka vitendo vya vurugu vinavyoweza kuhatarisha utulivu wa nchi kwa sababu wanaaminika kwa watu.

"Suala la amani halipaswi kuachwa kuzungumzwa, hata sasa wakati hali ya nchi inaonekana kuwa shwari, bali linapaswa kuendelea kusisitizwa ili jamii itambue umuhimu wa kulinda amani iliyopo," alisema Nahdi.

Kiongozi huyo ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kituo cha Uzingatiaji na Ushauri wa Huduma za Kifedha za Kiislamu (CIFCA) aliainisha mambo kadhaa ya kusisitizwa katika mahubiri ya maimamu ikiwemo umuhimu wa kuishi kwa upendo, kuheshimiana, maadili, mshikamano, kushirikiana na serikali na wananchi wenyewe kushirikiana katika mambo ya kijamii bila kujali tofauti zilizopo.

Nahdi alisema kutokana na ufahamu wa maimamu wa historia na uzefu wao wa kutembea katika kueneza dini, wanaweza kwa ufanisi mkubwa kutoa elimu inayosaidia jamii kutambua madhara ya migogoro na vitendo vya vurugu kupitia mifano ya jamii mbalimbali duniani.

Hata hivyo, kipekee alisisitiza zana muhimu maimamu wanapaswa kuitumia katika kuhubiri amani, upendo, tabia njema, maadili na mshikamano katika nchi ni ushahidi wa nguvu kutoka katika mafundisho ya dini, hususan Qur'an na Sunna kwa ufahamu wa wema waliotangulia.

Kwa upande wa taasisi yake, The Islamic Foundation, Nahdi alisema itaendelea kwa nguvu ileile na bila kuchoka, kushirikiana na Serikali katika masuala mbalimbali ya kuimarisha huduma za jamii kwa manufaa ya Watanzania wote, ikiwemo elimu, maji, malezi ya watoto yatima na huduma nyingine zinazolenga kuboresha maisha ya wananchi.

Lakini alisisitiza kuwa ni sera ya vyombo vya habari vya Imaan vivyomilikiwa na taasisi ya The Islamic Foundation kuhubiri amani, upendo, ushirikiano, maendeleo bila kusahau maadili mema yanayompendeza Allah Mtukufu.

RABIU UL THANI 18, 1448

ربيع ثان

AWQAF TANZANIA

MWANDISHI WETU

TISHIO LA EL NIÑO

Dkt. Kassim ajenga hoja kuanzishwe Waqf wa kuzuia majanga nchini

Mwenyekiti wa Awqaf Tanzania na mtaalamu wa fedha za Kiislamu, Dkt. Kassim Nurdin Hussein, amependekeza kuanzishwa kwa Waqf maalumu ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na majanga, akisema jamii inapaswa kuwekeza zaidi katika kuzuia madhara kabla hayajatokea badala ya kusubiri mafuriko ndipo kuanza kutafuta fedha za uokoaji.

Katika andiko lake la karibuni kuhusu Waqf, Dkt. Kassim amesema mfumo huo unaweza kutumika kujenga hazina ya kudumu itakayosaidia kugharamia hatua za tahadhari, makazi mbadala ya muda, vifaa vya dharura na msaada kwa familia maskini zinazoishi maeneo hatarishi.

"Je, tusubiri maji yafurike ndiyo tuanze kuwaokoa, au tuchukue hatua madhubuti sasa?" amehoji.

Amesema mabadiliko yanahitajika katika namna jamii inavyokabiliana na majanga, kutoka kutumia nguvu kubwa katika uokoaji baada ya madhara hadi kuweka rasilimali katika hatua zinazoweza kupunguza athari mapema.

El Niño yaongeza umuhimu wa maandalizi

Pendekezo hilo linakuja wakati Tanzania ikijiandaa kwa mvua za Vuli zinazotarajiwa kuathiriwa na El Niño.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilitangaza Agosti 18 kuwa msimu wa Oktoba hadi Desemba 2026 unatarajiwa kuathiriwa kwa kiwango kikubwa na El Niño yenye nguvu.

Mvua za juu ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya Pwani ya Kaskazini, Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki, Ukanda wa Ziwa Victoria na kaskazini mwa Kigoma, huku ongezeko kubwa la mvua likitarajiwa Novemba.

TMA imeonya kuhusu uwezekano wa mafuriko, kuongezeka kwa kina cha maji katika mito na mabwawa pamoja na athari nyingine zinazoweza kuambatana na mvua nyingi.

Kutokana na tahadhari hiyo, Serikali ilitoa maelekezo 13 kwa taasisi, mikoa na halmashauri, yakiwemo kutambua maeneo hatarishi, kufanya tathmini za hatari na kuwahamasisha wananchi kuhama kwenda maeneo salama inapohitajika.

Tatizo si kuhama tu, bali kwenda wapi?

Dkt. Kassim ametumia maeneo ya Kigogo na Jangwani, Dar es Salaam, kueleza changamoto inayowakabili wananchi wa kipato cha chini wanapoambiwa waondoke maeneo yanayoweza kukumbwa na mafuriko.

Maeneo mbalimbali katika Bonde la Msimbazi yana historia ya mafuriko, na "Serikali, kwa ushirikiano na washirika wa maendeleo, inaendelea kutekeleza hatua za kupunguza hatari ya mafuriko katika Bonde la Msimbazi."

Hata hivyo, kwa familia maskini, kuhama si uamuzi rahisi. Baadhi yao hutegemea biashara ndogo, wateja wa eneo walilopo au kazi za karibu. Kuhama mbali kunaweza kuongeza gharama za usafiri au kukatisha chanzo cha mapato.

Ndiyo maana Dkt. Kassim anapendekeza familia zilizo hatarini zisaidiwe kupata makazi salama ya muda, ikiwezekana yasiyo mbali sana na shughuli zao za kujipatia riziki. Vyumba vya kupanga katika maeneo salama vinaweza kutumika kama sehemu ya mpango huo.

Changamoto hiyo imeonekana pia Zanzibar, ambako Serikali imetambua shehia 188 za Unguja na Pemba zenye maeneo yanayoweza kukumbwa na madhara ya mvua kubwa. Wananchi wa maeneo hatarishi wamehimizwa kuhama, ingawa baadhi yao wameeleza kutokuwa na sehemu mbadala za kwenda.

Mkoani Pwani, viongozi pia wameelekeza wilaya na halmashauri kutenga maeneo yanayoweza kutumika kuwahifadhi wananchi watakaoathiriwa.

Waqf itafanyaje kazi?

Kwa mujibu wa pendekezo la Dkt. Kassim, fedha au mali zitawekwa katika Waqf na mapato yatakayozalishwa yatatumika kufadhili maandalizi ya majanga. Fedha hizo zinaweza kugharamia makazi ya muda, vifaa vya uokoaji, chakula, maji, huduma za msingi na misaada mingine kwa familia zilizo katika hatari.

Lengo ni kuwa na rasilimali zinazopatikana kabla ya maafa badala ya kuanza michango wakati nyumba tayari zimefurika na wananchi wamepoteza mali.

Pendekezo hilo pia linataka matumizi ya Waqf yavuke maeneo yaliyozoeleka kama ujenzi wa misikiti, visima na shughuli nyingine za kijamii, na kuingia katika ulinzi wa jamii dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi. Dhana ya kutumia Waqf katika masuala ya mazingira si mpya. Mwaka 2022, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Bodi ya Waqf ya Indonesia na washirika wengine waliandaa mwongozo wa Green Waqf, unaoeleza namna mali za Waqf zinavyoweza kusaidia miradi ya mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

MWANDISHI WETU



AMYC yaweka mkazo elimu inayoambatana na malezi ya kitabia

Mudir wa taasisi ya Ansar Muslim Youth Center (AMYC), Sheikh Salim Barahiyan, amesema taasisi hiyo imedhamiria kuwapatia vijana elimu sambamba na malezi ya kitabia ili kujenga kizazi chenye nidhamu na uwezo wa kukabiliana na changamoto za dunia ya sasa.

Akizungumza katika mahafali ya 16 ya Shule ya Msingi Muzdalifa wilayani Korogwe, mkoani Tanga, Sheikh Barahiyan alisema ni mkakati wa taasisi hiyo itatumia vituo vyake kuwaandaa vijana kwa kuwapatia maarifa ya dini na mazingira, huku wakijengewa misingi ya kumjua Mungu na kuthamini muda.

"Moja ya malengo makubwa ya taasisi hii ni kuwaelimisha vijana na Waislamu kwa ujumla kuhusu dini yao na elimu ya mazingira," alisema.

Alifafanua kuwa jitihada hizo zinalenga kumpa kijana msingi mpana wa elimu na malezi utakaomwezesha kukabiliana na changamoto za maisha huku akizingatia maadili.

Kwa upande wake, mgeni rasmi katika mahafali hayo, Hassan Mussa Shekivuli, amewataka Waislamu kushikamana na kuongeza kasi katika juhudi za maendeleo.

Shekivuli alisema mshikamano ni muhimu katika kufikia maendeleo kwa kasi ili kuziba pengo lililopo. "Kwa kweli tunatakiwa tushikamane ili kufikia maendeleo angalau nusu. Wenzetu wanatembea, sisi tunatakiwa tukimbie kwa sababu tumeachwa," alisema.

Nao wazazi wa wanafunzi waliohitimu wameeleza umuhimu wa ushirikiano kati ya shule, wazazi na jamii katika kuhakikisha watoto wanapata elimu bora inayokwenda sambamba na malezi, huku mmoja wao Hatibu Shekuwavu, akiasa jamii inapaswa kuunga mkono shule za Kiislamu zinazotoa elimu na kufundisha maadili.

"Tuwe mabalozi kule tuliko, tuwaambie kuwa Korogwe kuna shule inayotoa malezi ya kidini, maadili mema na elimu kuhusu mazingira," alisema Hatibu.

Rais Samia atajwa Marekani kinara afya na utu wa wanawake, watoto

Rais wa Namibia, Netumbo Nandi–Ndaitwah, amesifu juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kulinda afya na utu wa wanawake na watoto, akihusianisha na ujenzi wa mustakabali bora wa bara la Afrika.

Rais Ndaitwah alibainisha hayo jijini New York Marekani wakati wa mkutano ulioandaliwa na kinara wa Umoja wa Afrika katika Afya ya Mama na Mtoto, Rais Samia Suluhu Hassan kujadili "Uhamasishaji kwa ajili ya enzi mpya: Wanawake wanaoongoza katika afya ya mama na mtoto kwa wote".

Mkutano huo uiobatizwa SHE RISES ulifanyika pembezoni mwa Mkutano Mkuu wa 81 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA 81) jijini New York, Marekani.

Rais Ndaitwah alisema uwekezaji katika afya ya mama na mtoto ni uwekezaji katika watu, uchumi na maendeleo endelevu, huku akizitaka nchi za Afrika kuongeza uwezo wa ndani wa kugharamia huduma za afya ya mama na mtoto, badala ya kutegemea misaada ya nje pekee.

Wakati huo huo, viongozi na wadau wa afya duniani wameahidi kuendelea kuunga mkono juhudi za Tanzania za kuimarisha afya ya mama na mtoto, huku wakisisitiza umuhimu wa kuwashirikisha zaidi wanawake katika uongozi na maamuzi yanayohusu mifumo.

Katika hatua nyingine, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Deogratius Ndejembi amesema kuwa kupungua kwa vifo vya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano Tanzania ni ishara kuwa utashi wa kisiasa unapounganishwa na rasilimali na utekelezaji wa mipango iliyowekwa unaweza kuleta mabadiliko yanayogusa maisha ya wananchi moja kwa moja.

MAKALA
YA MAONI

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

Hongera Tanzania kuweka msimamo kutetea amani, haki kimataifa



Katika kipindi cha ujahili, Waarabu hawakuwa na mfumo maalumu wa kushughulikia tuhuma za uzinzi au kupinga nasaba ya mtoto. Baada ya kuja kwa Nabii Muhammad (rehema na amani ya Allah zimshukie), sharia ya kuapizana (li'aan) ilishushwa katika Sura ya 24, An–Nur, kwa lengo la kutatua migogoro hiyo kwa njia ya haki na inayolinda maslahi ya pande zote. Sharia hii inahusishwa na tukio la Hilal bin Umayya, ambaye alimtuhumu mkewe kwa uzinzi, lakini hakuwa na mashahidi wanne wa kuthibitisha tuhuma hizo. Ndipo Allah akashusha sharia ya kuapizana kama njia ya kisharia ya kushughulikia na kumaliza mgogoro huo.

Hongera Tanzania kuweka msimamo kutetea amani, haki kimataifa

Katika dunia inayoshuhudia migogoro, vita na mivutano inayozidi kugawa jamii na mataifa, kuna umuhimu mkubwa kwa nchi kusimama na kusisitiza kwamba tofauti hazipaswi kutatuliwa kwa nguvu bali mazungumzo na diplomasia katika hali ya kuheshimiana na kwa nia ya dhati ya kutafuta suluhisho linalozingatia utu wa binadamu.

Kwa mtazamo huu, ujumbe uliotolewa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Deogratius Ndejembi, alipomuwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika Mjadala Mkuu wa Kikao cha 81 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, ni ujumbe unaostahili kutafakariwa na kupongezwa.

Miongoni mwa maeneo muhimu yaliyogusiwa ni mgogoro wa muda mrefu wa Israel na Palestina, hususan hali ya Gaza na Mashariki ya Kati. Tanzania imesisitiza haja ya kuwalinda raia, kuhakikisha misaada ya kibinadamu inawafikia wanaohitaji bila vikwazo na kurejesha diplomasia kuwa njia kuu ya kutafuta amani ya kudumu.

Huu ni ujumbe unaogusa msingi wa utu: kwamba nyuma ya takwimu za vita kuna binadamu watoto, wanawake, wazee na familia zinazostahili kuishi kwa usalama na heshima.

Tanzania pia imerejea katika msimamo wake wa muda mrefu wa kuunga mkono suluhisho la nchi mbili, ambapo Israel na Palestina zinaishi pamoja kwa amani na usalama, kwa kuzingatia sheria za kimataifa na maazimio husika ya Umoja wa Mataifa. Aidha, Tanzania imesisitiza haki ya watu wa Palestina ya kujitawala.

Jambo la kuzingatia hapa ni kwamba Tanzania haijaiangalia Palestina kama suala la kisiasa pekee. Ujumbe uliotolewa unaliweka suala hilo pia katika muktadha wa utu, usalama wa raia, haki na amani ya kudumu.

Ni mtazamo unaokumbusha kwamba diplomasia si udhaifu. Mazungumzo si kushindwa. Na kutafuta suluhisho la amani si kuacha kusimamia haki. Kinyume chake, mazungumzo yenye msingi wa sheria, heshima na haki yanaweza kuwa njia ya kuzuia kizazi kingine kurithi migogoro ambayo imechukua miongo kadhaa bila suluhisho la kudumu.

Tanzania yenyewe imeeleza kuwa msimamo wake kuhusu Palestina umedumu kwa takribani miaka 50 na umejengwa katika misingi ya sera yake ya mambo ya nje.

Kwa hiyo, ujumbe wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa unaweza kutazamwa kama mwendelezo wa msimamo unaosisitiza dunia yenye nafasi zaidi kwa mazungumzo, ushirikiano wa kimataifa na utatuzi wa migogoro kwa njia za amani.

Katika kipindi ambacho dunia inahitaji si kuongeza sauti za uhasama, bali kuongeza sauti zinazowakumbusha viongozi wajibu wao kwa maisha ya watu, ujumbe wa Tanzania kuhusu amani, utu na diplomasia umeleta hoja muhimu kwenye jukwaa la kimataifa.

Ni wajibu wa jumuiya ya kimataifa kuendelea kutafuta njia zitakazomaliza mateso ya raia na kuwezesha suluhisho la kudumu, la haki na linaloheshimu sheria za kimataifa.

Amani ya kweli haijengwi kwa ushindi wa upande mmoja dhidi ya mwingine; hujengwa kwa kutafuta mazingira ambayo utu, usalama, haki na heshima vinaweza kuwa msingi wa maisha ya wote.

NA MRISHO TOZO

Magereza, The Islamic Foundation kuzidi kushirikiana kurekebisha wafungwa

JESHI la magereza mkoa wa Morogoro limesisitiza umuhimu wa kuendelea kuimarisha ushirikiano na taasisi ya The Islamic Foundation katika kusaidia kurekebisha wafungwa, kuwaandaa kurejea katika jamii na kuwawezesha kuanza maisha mapya baada ya kumaliza vifungo vyao.

Jeshi hilo limeeleza hayo baada ya kufanya ziara katika Makao Makuu ya taasisi ya The Islamic Foundation mjni Morogoro, pamoja na kutembelea vyombo vya habari vya Imaan - Radio Imaan na TV Imaan, katika ziara iliyofanyika tarehe 22 Septemba 2026 kwa lengo la kuimarisha ushirikiano na kutoa shukrani kwa wadau wanaochangia katika utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Magereza.

Akizungumza Mkuu wa Magereza na Mahabusu Morogoro, SP SabaSaba Mselemu, amesema ziara hiyo imefanyika kwa lengo la kuishukuru taasisi ya The Islamic Foundation na kipekee TV Imaan kwa ushirikiano wao katika kutekeleza jukumu la urekebishaji wa wafungwa.

SP SabaSaba Mselemu alisema The Islamic Foundation imekuwa mdau muhimu wa Jeshi la Magereza kwa kutoa vitabu vya dini vinavyotumika kuwasaidia wafungwa katika elimu ya dini na malezi kwa lengo la kuwaandaa kurejea katika jamii wakiwa raia wema.

Alisema ushirikiano huo hauishii katika utoaji wa vitabu vya dini, bali pia unahusisha kuwawezesha wafungwa wanaopata mafunzo mbalimbali wakiwa magerezani baada ya kumaliza vifungo vyao, akitolea mfano mfungwa mmoja aliyemaliza kifungo na kuhitimu mafunzo ya ushonaji pamoja na kupata cheti kutoka VETA.

SP SabaSaba Mselemu alisema baada ya mfungwa huyo kumaliza kifungo na kuhitimu mafunzo hayo, The Islamic Foundation ilimpatia cherehani ili aweze kuanza maisha mapya baada ya kutoka gerezani, hatua inayolenga kumsaidia kujitegemea na kuepuka kurejea katika makosa. Katika ziara hiyo, Jeshi la Magereza pia limetembelea Radio Imaan na TV Imaan, likisisitiza umuhimu wa vyombo hivyo kuendelea kuelimisha jamii kuhusu kazi zinazofanywa na Jeshi la Magereza, hususan katika urekebishaji, malezi na maandalizi ya wafungwa kurejea katika jamii, huku pande hizo zikisisitiza kuendelea kuimarisha ushirikiano katika shughuli zinazolenga kuwasaidia wafungwa na kuchangia maendeleo ya jamii.

Aref Nahdi: Ushirikiano umeanza mbali, akumbusha maji

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Mwenyekiti wa taasisi ya The Islamic Foundation, Aref Nahdi, alikumbusha kuwa taasisi hiyo imekuwa ikishirikiana na Jeshi la Magereza kwa muda mrefu katika kusaidia wafungwa na kuboresha mazingira yao, ikiwemo kuchangia upatikanaji wa huduma za maji kupitia uchimbaji wa visima.

Alisema The Islamic Foundation pia imekuwa ikishirikiana na Magereza katika kipindi cha mwezi wa Ramadhan kwa kutoa futari kwa wafungwa, pamoja na kusaidia baadhi ya wafungwa wenye makosa madogo ambao wanaweza kuachiwa baada ya kulipiwa faini zao kwa mujibu wa taratibu na sheria.

Nahdi alisema hatua ya kuwasaidia wafungwa wanaostahili kuachiwa baada ya kulipa faini inaweza kumwezesha mfungwa kurejea katika familia yake, huku pia ikisaidia kupunguza gharama zinazobebwa na Serikali katika kumhudumia mfungwa akiwa gerezani.

MIMBARI ZETU

IMEANDALIWA
Na Barnabas Mkwayu
0766 364 354

KUTOKA

Masjid Nurah
(Msamvu, Morogoro)

Masjid Al-Haram
(Makka)

Masjid Haqq
(Karume, Morogoro)

MIMBARI ZETU

MSIKITI MTAKATIFU, MAKKA
IMAM NA KHATIBU SHEIKH DKT. YASSER BIN RASHID AL-DOSARI

Waislamu waaswa kutumia vizuri muda, kuacha uvivu

Waislamu wametakiwa kuwa na hima kubwa katika mambo ya dini na dunia, kutumia kwa hekima muda wa maisha na fursa walizopewa na Mwenyezi Mungu, huku wakijiepusha na uvivu, kusita na tabia ya kuahirisha mambo.

Akitoa khutba ya Ijumaa katika Msikiti Mkuu wa Makkah, Septemba 25, 2026, Imam na Khatibu wa Msikiti huo, Sheikh Dkt. Yasser bin Rashid Al-Dosari, alisema kuwa hima ya juu ni miongoni mwa sifa zinazomuinua mwanadamu na kumlinda dhidi ya udhaifu, kukata tamaa na kushindwa kufikia malengo yake.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya Saudi Arabia, ikiwemo Sabq, Makka News na Media Post, Sheikh Al-Dosari alisema mafundisho ya Uislamu yanawahimiza waumini kushindana katika kufanya mema na kujitahidi kufikia viwango vya juu katika maisha ya dunia na Akhera.

Alisisitiza kuwa mwanadamu anapaswa kutambua thamani ya umri wake na kutumia vizuri kila fursa inayopatikana kabla haijapita. Alionya kuwa uvivu, kusita na kuendelea kuahirisha mambo kunaweza kumnyima mtu fursa muhimu za kufanikisha malengo yake.

Sheikh Al-Dosari alieleza kuwa kuwa na hima kubwa hakumaanishi mtu kuacha shughuli za dunia au kujitenga na maisha ya kawaida. Badala yake, alisema, ni kufanya kazi kwa bidii, kuwa na malengo yenye manufaa na kutafuta yaliyo bora katika masuala ya dini na maisha.

Alisema maendeleo ya jamii na mataifa yanategemea uwepo wa watu wenye malengo makubwa, dhamira thabiti, juhudi na uvumilivu katika kuyafikia.

Sheikh Al-Dosari aliwahimiza Waislamu kuutumia muda wao katika mambo yenye manufaa, kufanya mema kwa bidii na kutokubali maisha yao yatawaliwe na uzembe au kuahirisha wajibu.

MSIKITI WA MTUME, MADINA
IMAM NA KHATIBU SHEIKH DKT. SALAH AL-BUDAIR

Pepo haitafutwi kwa matarajio ya maneno, ni vitendo

Waumini wametakiwa kutofanya Pepo kuwa matarajio ya maneno pekee, bali kujitahidi kwa vitendo na kuongeza matendo mema yatakayowasogeza karibu na radhi za Mwenyezi Mungu na kuwaandalia maisha mema ya Akhera.

Akihutubu katika Msikiti wa Mtume mjini Madina, Septemba 25, 2026, Imam na Khatibu Sheikh Dkt. Salah Al-Budair aliwaeleza waumini kuhusu neema kubwa zilizotayarishwa kwa ajili ya waja wema katika Pepo, akiwahimiza kuongeza juhudi katika ibada na matendo mema.

Kwa mujibu wa Sabq, Makkah News na Media Post, Sheikh Al-Budair alisema Mwenyezi Mungu ameifanya Pepo kuwa makazi ya waja Wake wema, yenye rehema, heshima na neema zisizo na mwisho.

Alikumbusha hadith ya Mtume Muhammad (S.A.W) inayofafanua ukubwa wa neema hizo, kwamba Mwenyezi Mungu amewaandalia waja Wake wema mambo ambayo jicho halijawahi kuyaona, sikio halijawahi kuyasikia na moyo wa mwanadamu haujawahi kuyawaza.

Sheikh Al-Budair alisema Pepo ina milango minane, akiwahimiza Waislamu kumuomba Mwenyezi Mungu waingizwe katika Pepo ya Firdaus, ambayo ni miongoni mwa sehemu zake za juu.

Aidha, alieleza kuwa maisha ya Peponi yatakuwa tofauti kabisa na maisha ya dunia, kwani hakutakuwa na kifo, uzee wala maradhi. Waumini wataishi katika neema na usalama wa kudumu kwa idhini ya Mwenyezi Mungu.

Akisisitiza umuhimu wa kujiandaa kwa Akhera, Sheikh Al-Budair aliwataka Waislamu kutopoteza muda na fursa walizopewa katika maisha ya dunia, bali wazitumie kufanya ibada, kusaidia wengine na kutenda mema.

Alisema matarajio ya kupata Pepo yanapaswa kuambatana na juhudi za vitendo, kwani muumini anatakiwa kuonyesha imani yake kupitia utiifu kwa Mwenyezi Mungu na matendo mema.

MIMBARI ZETU

MASJID HAQQ, MOROGORO
SHEIKH IBRAHIM TWAHA

Shukrani ni mlango wa baraka na ongezeko la neema

MOROGORO — Sheikh Ibrahim Twaha, Mkurugenzi wa Taasisi ya The Islamic Foundation, amewataka Waislamu kuwa miongoni mwa wenye kumshukuru Allah Subhanahu wa Ta'ala kwa neema walizopewa, akisisitiza kuwa shukrani ni sababu ya kuongezewa neema na baraka.

Sheikh Ibrahim alitoa nasaha hizo, akieleza kuwa neno shukrani lina nafasi kubwa katika Uislamu na ni miongoni mwa maneno anayoyapenda Allah Subhanahu wa Ta'ala.

Alisema watu wamefanikiwa kulitumia neno hilo kwa usahihi na kujenga tabia ya kushukuru, jambo linalowafanya kutambuliwa kwa sifa hiyo njema. Kwa upande mwingine, alionya kuwa kutokuwa na shukrani ni miongoni mwa mambo yanayoweza kumweka mtu mbali na mapenzi ya Allah.

Sheikh Ibrahim alisema baadhi ya watu wamepata hasara kwa kupuuza neema walizopewa na kushindwa kuwa na shukrani, akiwataka Waislamu kutambua kuwa kila mmoja anahitaji ongezeko la neema kutoka kwa Allah.

Akirejea mafundisho ya Qur'ani, Sheikh Ibrahim alisema Allah Subhanahu wa Ta'ala ameahidi kuwa wenye kushukuru wataongezewa neema, akisisitiza kuwa ahadi hiyo inamhusu kila anayemshukuru Muumba wake kwa dhati.

"Nani mkiwa wenye shukrani, wenye kushukuru, Allah atakuzidishieni," alisema, akisisitiza umuhimu wa Waislamu kutafakari maana na matokeo ya shukrani katika maisha yao.

Kwa mujibu wa Sheikh Ibrahim, shukrani haileti tu ongezeko la neema, bali pia huambatana na baraka katika maisha ya mtu, ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa mali na kuwepushwa na mambo mbalimbali yenye madhara.

Alisema neema na mema ambayo mtu anayapata yanapaswa kuwa sababu ya kumrudisha zaidi kwa Allah kwa kumshukuru, badala ya kuyachukulia kuwa jambo la kawaida.

MASJID HAQQ, MOROGORO
SHEIKH HASHIM GEORGE

Uaminifu ni msingi wa mume bora katika maisha ya ndoa

MOROGORO — Sheikh Hashim George amewataka waume kuwa waaminifu, waadilifu na wenye kuheshimu haki za wake zao, akisema uaminifu na kuishi kwa wema ni miongoni mwa sifa zinazomtofautisha mume bora katika maisha ya ndoa.

Sheikh Hashim alitoa kauli hiyo katika khutba ya Ijumaa iliyotolewa katika Masjid Haqq, Karume mkoani Morogoro, iliyojikita katika kueleza sifa zinazopaswa kumpamba mume bora katika familia.

Alisema mume anatakiwa kuwa mtu wa amana, asiye na hiyana na anayelinda haki na heshima ya mke wake, akisisitiza kuwa mwanaume hapaswi kumdhulumu mke wake wala kutumia mali yake kwa njia isiyo halali.

Kwa mujibu wa Sheikh Hashim, changamoto nyingi zinazoikumba taasisi ya ndoa zinatokana na baadhi ya wanandoa kutoshughulika ipasavyo na wenza wao, kutoheshimu haki zao na kushindwa kutekeleza wajibu waliopewa. Alieleza kuwa mume bora ni yule anayejenga uhusiano mzuri na mke wake kwa kuheshimiana, kutendeana wema na kutekeleza haki na wajibu wa kila mmoja.

Sheikh Hashim alionya kuwa pale mume anapokuwa mwaminifu, mwenye huruma na anayemheshimu mke wake, hujenga mazingira yanayochochea utulivu na mshikamano ndani ya familia.

Akizungumzia umuhimu wa ndoa, Sheikh Hashim alisema ndoa ina nafasi ya pekee katika Uislamu kwa kuwa ni ibada yenye masharti na wajibu unaowekwa kwa wahusika tangu kabla ya kuingia katika maisha ya pamoja.

Alisisitiza kuwa waume wanapaswa kutambua kuwa kuishi vizuri na wake zao si suala la hiari, bali ni sehemu ya wajibu na mafungamano ambayo Uislamu umeyaweka kwa ajili ya kulinda heshima, haki na ustawi wa familia.

Alisema mume anayezingatia amana, haki, heshima na muamala mwema huweka msingi wa ndoa yenye utulivu na maisha ya familia yenye mshikamano.

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
0789 201383

Viongozi Zanzibar fanyieni kazi kauli hii ya Rais Mwinyi

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amesema maridhiano kati ya CCM na ACT–Wazalendo hayapaswi kuishia katika makubaliano ya kisiasa au uteuzi wa viongozi, bali yanapaswa kuzaa matokeo kwa kuharakisha maendeleo na kutatua changamoto zinazowakabili wananchi.

Dkt. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu Zanzibar wakati wa hafla ya kumuapisha Mwenyekiti wa ACT–Wazalendo, Othman Masoud Othman kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

“Maridhiano si mwisho wa safari, bali ni mwanzo wa kazi,” alisema Dkt. Mwinyi, akisisitiza umuhimu wa kuboresha huduma za kijamii na miundombinu, ikiwamo afya, elimu, maji na nishati.

Alisema maeneo hayo ndiyo yatakayowawezesha wananchi kuona matokeo ya maridhiano katika maisha yao ya kila siku.

Kwa upande wake, Othman alisema ni muhimu kuvumiliana licha ya kuwepo kwa tofauti za kisiasa. Akitoa mfano wa togwa, alisema kama maji na mtama vinavyohitaji kuchanganywa ili kutengeneza togwa, ndivyo Wazanzibari wanavyopaswa kukubali tofauti zao na kujenga utamaduni wa kuvumiliana.

Kauli hii inatukumbusha kuwa tofauti za kisiasa zipo katika jamii, lakini zinapaswa kushughulikiwa kwa mazungumzo, kuheshimiana na kutanguliza maslahi ya umma. Vivyo hivyo, watu wenye mitazamo tofauti wanaweza kushirikiana katika mambo yenye maslahi kwa umma bila kulazimika kufanana katika kila jambo.

Kwa kuzingatia uzito na unyeti wa suala hili, ni muhimu kudumisha umoja na mshikamano miongoni mwa Wazanzibari, kwani jamii imara hujengwa kwa ushirikiano, maelewano na uwajibikaji wa pamoja. Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) alipata kusema: “Muumini kwa muumini mwenzake ni kama jengo, sehemu moja huimarisha nyingine.” [Bukhari na Muslim].

Kwa hiyo, viongozi waliopewa dhamana ya kuwaongoza Wazanzibari watambue kuwa wananchi hawahitaji tu kuwaona wakishirikiana katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa, bali wanataka kuona matokeo ya umoja huo katika maisha yao.

Maridhiano hayapaswi kuwa makubaliano ya kisiasa pekee, bali yawe msingi wa kuboresha maisha na ustawi wa Wazanzibari. Umoja wa kisiasa ukiambatana na uwajibikaji, haki na maendeleo, ndipo maridhiano yatakapokuwa na maana halisi kwa wananchi.

فتاوى

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

Je, napaswa kutoa zaka ya hisa ninazomiliki katika kampuni ya biashara?

Swali: **Mtu alinunua kitabu, kisha akakuta kimeandikwa juu yake "Waqfu", afanye nini?**

Jibu: Aende kwa muuzaji na amweleze kuwa kitabu hicho ni Waqf, hivyo hakiruhusiwi kuuzwa. Kwa hiyo, mkataba wa mauziano unavunjika, kwa sababu imebainika kuwa mauziano hayo hayakuwa sahihi. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

Swali: **Muulizaji anasema: Nina hisa katika kampuni ya kibiashara. Je, zaka inawajibika juu ya hisa hizo au la?**

Jibu: Hisa ni sehemu ya mtaji ambayo mshirika huichangia katika kampuni za hisa. Hisa hiyo inawakilisha sehemu maalumu ya mtaji wa kampuni. Kwa hiyo, kwa asili hisa ni mali, ingawa baadhi ya hisa zinaweza kuwa katika mfumo wa mali halisi ('ayn). Na kwa kuwa hisa ni mali inayomilikiwa, zaka inawajibika juu yake pale vigezo na masharti ya kuwajibika kwa zaka yanapotimia. Haya ndiyo yaliyokubaliwa na wanazuoni wa zama hizi.

Miongoni mwa wanazuoni hao, kuna wanaoona kwamba zaka ya hisa inapaswa kutolewa na mwenye hisa mwenyewe, kwa sababu yeye ndiye mmiliki wa hisa hizo; hivyo anatakiwa kutoa zaka yake.

Na miongoni mwao kuna wanaoona kwamba kampuni ndiyo inayopaswa kutoa zaka ya hisa kwa sababu kampuni ina dhima/shakhsiya ya kisheria inayojitegemea. Walisema, zaka ni haki inayohusiana na mali yenyewe, si lazima kila mara anayelazimika kuitoa awe mtu mwenye sifa za kuwajibika kisheria kidini. Hali hii inafanana na ulazima wa kutoa zaka katika mali ya mtoto mdogo au mtu mwenye wazimu.

Baadhi ya wanazuoni wameunganisha rai hizi mbili, wakasema kwamba zaka ya hisa kimsingi inamwajibikia mwenye hisa, kwa sababu yeye ndiye mmiliki halisi wa hisa; lakini kampuni inaweza kutoa zaka kwa niaba yake. Kwa hiyo, ikiwa kanuni za msingi za kampuni (mfumo wa kampuni) zimeeleza kwamba kampuni ndiyo inayotoa zaka ya hisa, basi kampuni itatoa zaka hiyo, na wanahisa hawatadaiwa kuitoa tena wao wenyewe.

Lakini ikiwa kampuni haitoi zaka, basi mwenye hisa anatakiwa kutoa zaka ya hisa zake mwenyewe. Hii ni rai nzuri ambayo imepitishwa na Majma' al-Fiqh al-Islami huko Jeddah, Saudi Arabia.

Kampuni inapotoa zaka ya hisa, basi inapaswa kuhesabu zaka hiyo kwa namna ambayo mtu binafsi angehesabu zaka ya mali yake. Maana yake ni kwamba mali zote za wanahisa zinachukuliwa kwa upande wa zaka kama mali ya mtu mmoja, kisha zaka inatolewa kwa msingi huo, kwa kuzingatia kanuni ya khultwah (kuunganishwa kwa mali katika hukumu ya zaka) kwa mujibu wa wanazuoni wanaopanua matumizi ya kanuni hiyo katika aina zote za mali.

Hisa za kampuni ya kibiashara zinachukuliwa kama bidhaa za biashara ('Urudh at-Tijarah), hivyo thamani ya hisa hizo pamoja na faida zake huhesabiwa na kutolewa zaka kila mwaka kwa kiwango cha 2.5%.

Ama ikiwa mtu ni mwanahisa katika kampuni ya kibiashara na kampuni haitoi zaka, basi wajibu wa mwanahisa ni kutoa zaka ya hisa zake mwenyewe, baada ya kujua thamani ya hisa zake pamoja na faida iliyopatikana. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

Serikali yazidi kujipanga kuikabili athari za El niño

Serikali inaendelea kuratibu na kuongeza jitihada mbalimbali za kulinda maisha ya watu na mali kutokana na athari zinazoweza kusababishwa na El Niño, huku taasisi za kitaifa, mikoa na halmashauri zikichukua hatua za tahadhari kabla ya mvua kubwa.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imetabiri msimu wa Vuli wa Oktoba–Desemba 2026 kuathiriwa kwa kiwango kikubwa na El Niño yenye nguvu. Hali hiyo inahusishwa na ongezeko la joto la bahari katika Pasifiki ambalo hubadili mifumo ya mvua.

Mvua za juu ya wastani hadi wastani zinatarajiwa Pwani ya Kaskazini, Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki, Ukanda wa Ziwa Victoria na kaskazini mwa Kigoma. Ongezeko kubwa la mvua linatarajiwa Novemba.

Kitaifa, Ofisi ya Waziri Mkuu ilishatoa maelekezo 13 kwa wizara, taasisi, mikoa na halmashauri, yakiwemo kutambua maeneo hatarishi, kufanya tathmini za vihatarishi, kuwahamisha wananchi kutoka maeneo yasiyo salama na kuandaa vifaa vya uokoaji na huduma za dharura.

Katika sekta ya barabara, TANROADS imeanza ukaguzi na matengenezo ya madaraja, makalavati na mifereji. Kilimanjaro, maandalizi yamejikita Mwanga na Same, ikiwemo kusafisha njia za maji na kuimarisha Daraja la Makanya.

Dar es Salaam, Waziri wa Maji Jumaa Aweso Septemba 25 alikagua miundombinu ya DAWASA, ikiwemo Mpiji, kuhakikisha mifumo ya maji na usafi wa mazingira inalindwa dhidi ya mafuriko na uchafuzi.

Kanda ya Ziwa, TASAC imeendesha elimu Mwanza na Kagera kwa waendeshaji na watumiaji wa vyombo vya majini, ikisisitiza matumizi ya jaketi okozi na kufuatilia taarifa za TMA kabla ya safari.

Serikali pia imebadili ratiba ya mitihani kadhaa ya kitaifa, ikisogeza baadhi kutoka Novemba hadi Oktoba ili kupunguza uwezekano wa mvua kubwa na mafuriko kuvuruga usafiri na kufikiwa kwa vituo vya mitihani.

Tanzania yatwaa tuzo 3 ACI Africa Awards

Tanzania imeng'ara katika sekta ya usafiri wa anga barani Afrika baada ya Viwanja vya Ndege vya Kimataifa vya Julius Nyerere (JNIA) na Kilimanjaro (KIA) kutwaa tuzo tatu.

Katika tuzo za ACI Africa 2026, JNIA imetwaa tuzo mbili, ikiwamo nafasi ya pili katika kipengele cha Utawala Bora, chini ya Tuzo ya Ubora wa Uwezeshaji na Utayari wa Huduma kwa Abiria 2026 (Passenger Facilitation and Readiness Excellence Awards 2026).

Uwanja huo pia umeshika nafasi ya pili katika kipengele cha Ubunifu na Mageuzi ya Kiteknolojia (Innovation & Transformation) kwa kundi la viwanja vinavyohudumia kati ya abiria milioni mbili na milioni tano kwa mwaka.

Kwa upande wa KIA, uwanja huo umeibuka mshindi wa kwanza katika kipengele cha Ushirikishwaji wa Wadau (Stakeholder Engagement) chini ya Tuzo ya Uwezeshaji na Utayari wa Huduma kwa Abiria 2026, kwa kundi la viwanja vinavyohudumia chini ya abiria milioni mbili kwa mwaka.

Tuzo hizo zimepokelewa na Mkurugenzi wa Biashara na Maendeleo wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), Mzee Kilele kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TAA, Abdul Mombokaleo.

Hafla hiyo ilifanyika jijini Abuja, Nigeria wakati wa Mkutano Mkuu wa 35 wa Baraza la Viwanja vya Ndege Afrika (ACI Africa) uliofanyika kuanzia Septemba 19 hadi 25, 2026.

Mkutano huo uliobeba kaulimbiu "Next–Gen Airports: Driving Performance and Resilience", ulijadili mikakati ya kuimarisha utendaji, ubunifu, matumizi ya teknolojia na ustahimilivu wa viwanja vya ndege barani Afrika.

NA YUSUFU AHMADI, LUSHOTO

Jamii yatakiwa kutafakari mmomonyoko wa maadili

Jamii imetakiwa kutafakari sababu za mmomonyoko wa maadili na kuchukua hatua madhubuti, ikiwemo kuwapeleka watoto katika shule za dini, ili kuwajenga katika misingi ya maadili, nidhamu na uwajibikaji.

Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi ya Direct Aid Society Mkoa wa Tanga, Sheikh Mohamed Abbas Athuman alitoa wito huo katika mahafali ya Shule ya Awali na Msingi ya Kiislamu ya Jumuiya ya Wafanyakazi Waislamu wa Wilaya ya Lushoto (JUWWALU), yaliyofanyika Lushoto mkoani Tanga.

Sheikh Athuman alisema jamii inapaswa kujiuliza ilikosea wapi na kuchukua hatua za kukabiliana na changamoto ya mmomonyoko wa maadili, akidokeza kuwa matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii yanachangia mienendo mibaya ya vijana.

"Tujiulize tulikosea wapi mpaka maadili yanaporomoka, yanaharibika Jamii inaharibika kwa kuiga mambo yasiyofaa kutoka kwa wasanii na kupitia mitandao ya kijamii," alisema Sheikh Athuman.

Msomi huyo alisema elimu yenye manufaa ina nafasi muhimu katika kujenga jamii yenye ustaarabu na maadili, akisisitiza kuwa suala la maadili ni jukumu la jamii nzima na si la mtu, dini, dhehebu au kabila moja.

"Suala la maadili ni suala la jamii nzima, si la mtu au dini moja tu. Linahusu jamii yote ya Tanzania," alisema Sheikh Athuman.

Akisisitiza umuhimu wa elimu ya dini katika malezi ya watoto, Sheikh Athumani alisema mwongozo wa dini unasaidia kuwajenga watoto katika misingi ya maadili na mwenendo mwema.

"Hakuna jambo linaloweza kufanyika kwa usahihi bila kuwa na mwongozo. Kwa upande wetu Waislamu, mwongozo wetu ni Kitabu cha Allah na Sunna za Mtume, ambavyo walimu wanavitumia kuwaongoza watoto," alisema na kuongeza kuwa elimu yenye manufaa ni nyenzo muhimu katika kujenga jamii yenye ustaarabu na maendeleo endelevu.

Kwa upande wake, Katibu wa Msikiti wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Wilaya ya Lushoto, Sheikh Ismail Pangaleli aliwahimiza wazazi kuwapeleka watoto katika shule za kidini ili kuwajenga katika nidhamu, ambayo ni msingi muhimu wa mafanikio.

Naye Mkuu wa Shule ya JUWWALu, Bi. Zuena Saleh Shemdoe, amesema shule hiyo imeendelea kuweka mkazo katika utoaji wa elimu bora ili kumjenga mtoto kielimu, kinidhamu na kimaadili.

Kwa upande wake, Mthibiti Ubora wa Shule wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, Bi. Mary Maula, amesema shule za dini zina mchango katika malezi ya watoto kwa kuwajenga katika misingi ya imani na maadili.

"Shule hizi za dini zinawalea watoto katika misingi ya kiimani. Tunaamini shule hizi zinasaidia hata taifa, kwa sababu watu wanapokuwa na hofu ya Mungu, hatutarajii kuwa watakuwa majambazi au watoto wenye tabia zisizopendeza," alisema Bi. Maula.

Mahafali hayo yalikuwa ni ya awamu ya pili tangu kuanzishwa kwa shule hiyo na yalipambwa na shughuli mbalimbali, ikiwemo maigizo, ngonjera pamoja na maonesho ya kitaaluma yaliyoandaliwa na shule.

NA Mahmoud Nyamguma

Robo familia za Gaza zinaongozwa na wanawake

Takribani kaya 86,290 Gaza zinaongozwa na wanawake, karibu mara mbili ya kabla ya Oktoba 2023, wengi wakiwa wajane au waume zao wamepotea, wamezuiliwa, kujeruhiwa au kutoweka.

Wanawake sasa wanaongoza karibu familia moja kati ya nne katika Ukanda wa Gaza, huku vita vikibadilisha kwa kiasi kikubwa muundo wa familia na kuongeza mzigo wa maisha kwa wanawake.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu Masuala ya Kibinadamu (OCHA), ikinukuu uchambuzi mpya wa UN Women, takribani kaya 86,290 Gaza zinaongozwa na wanawake, karibu mara mbili ya kiwango cha kabla ya Oktoba 2023.

Wanawake hao ni pamoja na wajane na wale ambao waume zao hawajulikani walipo, wamezuiliwa, wamejeruhiwa vibaya au wametoweka.

UN Women imebaini kuwa karibu wanawake saba kati ya 10 wanaoongoza kaya hawana makazi yanayofaa, ikilinganishwa na asilimia 55 ya kaya zinazoongozwa na wanaume.

Aidha, robo tatu ya kaya zinazoongozwa na wanawake zimeripoti nyumba zao kuharibiwa, huku familia hizo zikilazimika kuhama kwa wastani mara nane tangu Oktoba 2023.

OCHA imesema hali hiyo imeongeza mzigo wa wanawake katika kutafuta chakula, maji, makazi na huduma muhimu kwa familia zao.

Shule 9 za Kiislamu Canada zatishiwa mauaji

Shule 9 za Kiislamu nchini Canada zimewekwa katika ulinzi mkali baada ya kupokea barua pepe isiyojulikana iliyotishia "kuwachinja" Waislamu na kudai Canada iwe "huru na Uislamu."

Barua hiyo ilisambazwa ndani ya saa 24 kwa shule zilizopo Ontario, British Columbia na Quebec, huku polisi katika maeneo hayo wakianza uchunguzi wa tukio la chuki dhidi ya Waislamu huku hofuzikipanda miongoni mwa familia za Kiislamu wakihofia usalama wa watoto wao., tovuti ya Global news inaripoti.

Chama cha Waislamu Canada (MAC) kimeongeza ulinzi katika shule hizo, huku polisi wa Peel wakiongeza doria karibu na misikiti na shule na kitengo chao cha uhalifu wa chuki kikichunguza.

Polisi wa Ottawa wamesema hadi sasa hakuna dalili ya tishio maalum au la haraka.

Tovuti ya Statistics Canada inaonyesha kuwa matukio ya uhalifu wa chuki yaliyolenga Waislamu yaliongezeka kutoka 84 mwaka 2020 hadi 229 mwaka 2024, ongezeko la takribani asilimia 173; kwa mwaka 2024 pekee, Waislamu walilengwa katika matukio 229, sawa na asilimia 17 ya uhalifu wote wa chuki uliolenga dini.

ربيع ثان

NA Mahmoud Nyamguma

El Niño yaongeza hofu ya njaa, utapiamlo zaidi Somalia

Mamilioni ya watu nchini Somalia wako katika hatari ya kukabiliwa na njaa kali na utapiamlo katika miezi ijayo kutokana na mafuriko yanayotarajiwa pamoja na upungufu wa fedha za misaada ya kibinadamu.

Kwa mujibu wa UNICEF, Serikali ya Somalia na Umoja wa Mataifa zimeonya kuwa watu milioni 5.4 wanatarajiwa kukabili kiwango cha mgogoro wa chakula au zaidi kati ya Oktoba na Desemba 2026, huku milioni 1.5 wakiwa katika kiwango cha dharura au zaidi.

Watoto ndio walio katika hatari kubwa zaidi. Takribani watoto milioni 1.92 wenye umri chini ya miaka mitano wanatarajiwa kuhitaji matibabu ya utapiamlo mkali kati ya Julai 2026 na Juni 2027, wakiwemo 433,000 wenye utapiamlo mkali zaidi.

Mafuriko yanayohusishwa na El Niño yanatarajiwa kuathiri watu milioni 2.5 hadi 3.5 na yanaweza kuwalazimisha takribani watu milioni moja kuhama makazi yao.

UNICEF, WFP na FAO zimesema fedha za haraka zinahitajika kuhakikisha chakula, matibabu, maji safi na huduma za lishe zinawafikia wananchi kabla barabara hazijakatika kutokana na mafuriko.

Wanawake Australia kupatiwa elimu ya afya misikitini

Misikiti nchini Australia imeanza kutumika zaidi kutoa elimu ya afya ya uzazi kwa wanawake Waislamu, baada ya utafiti kuonesha kuwa mazingira yanayozingatia imani na faragha yanawasaidia kupata taarifa kwa urahisi zaidi.

Kwa mujibu wa shirika la Muslim Network, mradi wa miaka miwili wa WARDA umeendesha warsha 26 katika misikiti na jumuiya za Kiislamu New South Wales, ukiwafikia wanawake 490 kutoka nchi 33 na lugha 21.

Takribani theluthi mbili ya washiriki walitoka maeneo yenye changamoto kubwa za kijamii, huku asilimia 82 wakisema walikusudia kubadili baadhi ya mienendo yao baada ya kupata elimu hiyo.

Siasa za mrengo wa kulia Ulaya zawaweka njia panda wahamiaji Waislamu

Baada ya kukimbia vita na kujenga maisha mapya Ujerumani, baadhi ya wahamiaji kutoka nchi za Kiislamu na Kiarabu sasa wako njia panda: kubaki katika nchi waliyoifanya makazi yao au kutafuta mahali pengine kutokana na kuongezeka kwa hisia dhidi ya wageni.

Reuters wanatoa mfano wa Shahd Najeeb na mumewe Mahmoud Hmouech waliokimbia Deir al-Zor, Syria, wakati wa vita vya wenyewe kwa wenyewe na kuanza upya maisha Rostock. Mahmoud anafanya kazi katika saluni ya kunyoa, huku Shahd akihudumia chakula katika shule. Wana watoto wawili.

Familia hiyo ni sehemu ya zaidi ya Wasyria 900,000 wanaoishi Ujerumani, wengi wao waliwasili kama waomba hifadhi.

Hata hivyo, kuongezeka kwa nguvu za chama cha Alternative for Germany (AfD), kinachosisitiza kupunguza uhamiaji, kumefanya baadhi ya wahamiaji kuhofia mustakabali wao.

Reuters ilizungumza na watu 20 wenye asili ya uhamiaji katika miji ya Rostock na Schwerin, wengi wakisema wameona ongezeko la kauli na vitendo dhidi ya wageni.

ربيع ثان

TAFAKURI YA WIKI

NA SAMRATH MSUYA
0789 201 383

Je miundombinu ya misikiti yetu ni rafiki kwa walemavu?

Katika miji na vijiji vya Tanzania, tunaendelea kuona misikiti mipya ikijengwa kwa juhudi kubwa za waumini. Hilo ni jambo jema. Lakini kuna swali moja ambalo halipaswi kubaki pembeni: Je, msikiti wetu unamruhusu kila Muislamu kuingia, kuswali, kusikiliza khutba na kushiriki shughuli zake kwa heshima na uhuru?

Kwa mwenye kutumia kiti cha magurudumu, jibu linaweza kuamuliwa na ngazi moja isiyo na njia panda. Kwa mwenye uoni hafifu, linaweza kuamuliwa na njia isiyo salama. Kwa mwenye ulemavu wa kusikia, khutba inaweza kuisha bila ujumbe kumfikia. Kwa mtoto mwenye usonji, sauti kubwa na msongamano vinaweza kufanya msikiti kuwa mahali pa hofu badala ya utulivu.

Hili si suala la kundi dogo. Uislamu unatufundisha kusimama imara kwa uadilifu; kwa hiyo, ufikivu wa nyumba za ibada si pambo, bali sehemu ya kuwapa watu haki ya kuabudu.

Sensa ya Watu na Makazi ya 2022 inaonyesha Tanzania ilikuwa na watu zaidi ya milioni 5.3 wenye umri wa miaka saba na kuendelea wanaoishi na aina fulani ya ulemavu, sawa na asilimia 11.2 ya watu katika kundi hilo. Changamoto ya kuona ndiyo iliyoongoza kwa asilimia 3, ikifuatiwa na kutembea kwa asilimia 1.7.

Hatuna takwimu ya kitaifa niliyoipata inayokagua misikiti ya Tanzania na kutuambia mingapi inafikika kwa urahisi na watu wenye ulemavu. Hivyo, si sahihi kutoa hukumu kwamba "misikiti mingi" haifikiki. Lakini tunayo sababu ya kujitathmini. Sera ya Taifa ya Ulemavu ya mwaka 2004 ilitaja ngazi, milango myembamba na vyoo visivyofikika kuwa miongoni mwa vikwazo katika majengo ya umma.

Sheria nayo inaweka mwelekeo. Tanzania Bara, Sheria ya Watu wenye Ulemavu inataka majengo mapya na ukarabati wa majengo ya zamani uzingatie ufikivu. Zanzibar, Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya 2022 nayo inataka wasanifu na wajenzi kuzingatia ufikivu tangu hatua ya usanifu.

Lakini sheria peke yake haitoshi. Tunahitaji kubadili namna tunavyofikiri kuhusu msikiti: maegesho yanayofikika, njia zisizo na ngazi au zenye njia panda salama, milango mipana, vyoo vinavyoweza kutumiwa na mwenye kiti cha magurudumu, viti vya kuswalia na njia salama kuelekea sehemu ya udhu.

Lakini mahitaji hayaishii hapo. Msikiti jumuishi unaweza kuwa na Qur'an ya nukta nundu, maandishi yenye herufi kubwa, mkalimani wa lugha ya alama katika matukio muhimu, mfumo wa sauti unaoweza kurekebishwa na sehemu tulivu kwa watu wanaozidiwa na kelele au msongamano. Kwa watoto wenye usonji au changamoto nyingine za ukuaji, chumba kidogo tulivu kinaweza kuwa tofauti kati ya familia kushiriki ibada na familia kuacha kabisa kuja msikitini.

Ulemavu hauonekani kila wakati. Mtu anaweza kusikia kwa shida, kuwa na changamoto ya utambuzi, afya ya akili au usonji bila sisi kujua. Kumtazama vibaya mtoto anayeshindwa kukaa kimya, au kumkemea mzazi wake, kunaweza kuwa kizuizi kikubwa kuliko ngazi.

Uzoefu wa taasisi ya Muhsen nchini Marekani unaonyesha kuwa misikiti inaweza kubadilika kwa makusudi. Zaidi ya misikiti 110 imepata uthibitisho wake wa kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu, unaojumuisha miundombinu na namna programu zinavyoendeshwa. Funzo ni kwamba ufikivu unaweza kupangwa, kupimwa na kuboreshwa.

Kwa misikiti mipya Tanzania, ujumbe ni rahisi: msisubiri jengo likamilike ndipo muanze kufikiria njia panda. Mshirikishe mhandisi, mbunifu na watu wenye ulemavu tangu mwanzo.

Kwa misikiti ya zamani, kutokuwa na fedha za ukarabati mkubwa si sababu ya kutofanya chochote. Inawezekana kuanza hatua kwa hatua: kuongeza njia panda salama, kuweka kishikio chooni, kupanua mlango mmoja, kuweka viti, kuboresha mwanga na alama, kuondoa vizuizi kwenye njia au kutenga eneo tulivu.

Lakini ukarabati wa kweli unapaswa pia kufanyika kwenye mitazamo yetu. Kamati za misikiti zinaweza kuwashirikisha watu wenye ulemavu na familia zao katika maamuzi, kuwafundisha wahudumu na vijana wa kujitolea namna ya kusaidia kwa heshima, na kuwapa watu wenye ulemavu nafasi katika uongozi badala ya kuwaona daima kama wapokeaji wa msaada.

Msikiti ni nyumba ya ibada, elimu na jamii. Ikiwa mtu anahitaji kubebwa juu ya ngazi ili aingie, kiziwi hawezi kufuatilia ujumbe, au familia yenye mtoto mwenye usonji inaona bora ibaki nyumbani, basi tuna kazi ya kufanya.

Tunapochangisha fedha kujenga msikiti mpya, tuongeze swali moja kwenye michoro yetu: Je, kila mmoja anaweza kuingia hapa?

DARASA LA WIKI

SEHEMU YA 1

SHEIKH
Seif Ruga
0712 690 811

Fahamu sharia na utaratibu wa kuapizana kwa wanandoa



Katika kipindi cha ujahili, Waarabu hawakuwa na mfumo maalumu wa kushughulikia tuhuma za uzinzi au kupinga nasaba ya mtoto. Baada ya kuja kwa Nabii Muhammad (rehema na amani ya Allah zimshukie), sharia ya kuapizana (li‘aan) ilishushwa katika Sura ya 24, An–Nur, kwa lengo la kutatua migogoro hiyo kwa njia ya haki na inayolinda maslahi ya pande zote. Sharia hii inahusishwa na tukio la Hilal bin Umayya, ambaye alimtuhumu mkewe kwa uzinzi, lakini hakuwa na mashahidi wanne wa kuthibitisha tuhuma hizo. Ndipo Allah akashusha sharia ya kuapizana kama njia ya kisharia ya kushughulikia na kumaliza mgogoro huo.

Fahamu sharia na utaratibu wa kuapizana kwa wanandoa

Katika kipindi cha ujahili, Waarabu hawakuwa na mfumo maalumu wa kushughulikia tuhuma za uzinzi au kupinga nasaba ya mtoto. Baada ya kuja kwa Nabii Muhammad (rehema na amani ya Allah zimshukie), sharia ya kuapizana (li'aan) ilishushwa katika Sura ya 24, An–Nur, kwa lengo la kutatua migogoro hiyo kwa njia ya haki na inayolinda maslahi ya pande zote.

Sharia hii inahusishwa na tukio la Hilal bin Umayya, ambaye alimtuhumu mkewe kwa uzinzi, lakini hakuwa na mashahidi wanne wa kuthibitisha tuhuma hizo. Ndipo Allah akashusha sharia ya kuapizana kama njia ya kisharia ya kushughulikia na kumaliza mgogoro huo.

Lengo la msingi la sharia hii ni kulinda heshima na hadhi ya mwanamke ili mume asimdhulumu kwa kumtuhumu bila kuwa na ushahidi wa kutosha.

Pili, sharia hii inalenga kuweka utaratibu wa kuthibitisha ukweli au uongo kwa pande zote mbili kupitia viapo vya kisharia, badala ya kutegemea tuhuma zisizo na ushahidi. Tatu, inalenga kumaliza migogoro ya kifamilia kwa njia ya kisharia na ya haki, badala ya kuruhusu migogoro hiyo kuendelea kwa msingi wa hisia na dhana.

Nne, kulinda nasaba ya mtoto kwa kuhakikisha kuwa uhusiano kati ya baba na mtoto hauharibiwi na tuhuma zisizo na uthibitisho. Tano, kulinda familia na jamii kwa ujumla kwa kudhibiti matumizi ya tuhuma na kupunguza machafuko ya kijamii yanayoweza kusababishwa na kashfa na uzushi.

Uislamu umeweka mkazo mkubwa katika kulinda familia isiangamie. Hata hivyo, pale maisha ya ndoa yanaposhindikana, talaka au kutengana huwa ndiyo suluhisho bora zaidi.

Mume anapomshutumu mkewe kwa uzinzi, na mke naye akakanusha tuhuma hizo na kusema mume ni mwongo, katika mazingira hayo sharia ya kuapizana (li'aan) kati ya mume na mke hutekelezwa.

Baada ya mchakato huo kukamilika, wanandoa hutengana na hawaruhusiwi kurudiana tena. Aya za Qur'an zinaonesha kuwa mchakato wa kuapizana hutokea katika hali kuu mbili.

Kwanza, pale mume anapomshutumu mkewe kwa uzinzi, lakini hana mashahidi wanne wa kuthibitisha tuhuma hizo. Pili, pale mume anapokataa ujauzito au mtoto kwa madai kwamba hakuwahi kumuingilia mkewe, au kwamba mimba hiyo si yake kwa sababu muda wa ujauzito ni mfupi kuliko muda unaokubalika kisharia.

Uislamu umeweka mfumo huu kama njia ya kisharia ya kulinda haki za wanandoa, kuhifadhi heshima za watu na kuzuia dhuluma, huku ukipinga taratibu maalumu na viapo vizito ili kuhakikisha kuwa jambo hili halitumiki kwa uongo au uonevu.

Uaminifu katika ndoa ni miongoni mwa haki zinazotokana na mkataba wa ndoa. Haki hii ni ya mume kwa mke wake, kwa kuwa mke ni sehemu ya "kitanda cha ndoa," na watoto wanaozaliwa huhusishwa na mume huyo.

Aidha, mume ana wajibu wa kuwapatia watoto wake chakula, malezi bora na kuishi nao kwa wema. Kumwingiza mtu wa nje katika nasaba ya mume kwa njia ya uzinzi ni miongoni mwa madhambi makubwa, na kunaweza kuwa sababu ya kuvuruga familia na kuchochea chuki na uadui katika jamii.

Kwa sababu hiyo, Uislamu umempa mume haki ya kuhakikisha uaminifu wa mkewe na kumzuia kufanya uchafu. Iwapo kuna ushahidi wa wazi wa kufanyika kwa uovu, mume ana haki ya kuwasilisha tuhuma hizo kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Uislamu.

Katika sharia ya Kiislamu, kumtuhumu mtu kwa uzinzi ni jambo zito sana. Allah Mtukufu ameweka adhabu kali kwa mtu anayemzushia mwingine tuhuma hii bila ushahidi.

Mtu huyo anatakiwa alete mashahidi wanne walioshuhudia waziwazi tukio hilo. Ikiwa hataleta mashahidi hao, atapigwa viboko 80 na ushahidi wake hautakubaliwa tena, na atahesabiwa kuwa miongoni mwa watu waovu.

Hata hivyo, wakati mwingine suala hilo huwa gumu, hasa kwa mume anayehisi kuwa mkewe amezini lakini hana uwezo wa kuleta mashahidi wanne.

Kwa sababu mume anahusika moja kwa moja na maisha ya ndoa yake, sharia ya Kiislamu imemruhusu kueleza tuhuma yake bila kufanyiwa hukumu ya kashfa ikiwa hana ushahidi. Utaratibu huo ndio unaojulikana katika sharia ya Kiislamu kama kuapizana (li'aan).

Ikiwa mume atamtuhumu mkewe kwa uzinzi bila kuwa na mashahidi wa kuthibitisha tuhuma hiyo, mke huyo huitwa mbele ya Hakimu (Kadhi) na kukumbushwa kumcha Allah Mtukufu.

Katika hatua hiyo, mke anaweza kukiri tuhuma alizotuhumiwa na mumewe. Ikiwa atakiri, hukumu ya kisharia inayomhusu mwanamke aliye katika ndoa ambaye amethibitika kufanya uzinzi itatekelezwa dhidi yake kwa mujibu wa taratibu za sharia.

Na iwapo atapinga na kukanusha tuhuma hizo, shauri hilo halitaishia hapo.

Itaendelea katika toleo lijalo



Malaysia yataka ushirikiano zaidi kukuza uchumi halal duniani

Malaysia imetoa wito wa kuimarishwa kwa ushirikiano wa kimataifa ili kupanua uchumi wa halal na kuongeza biashara, uwekezaji, ajira na upatikanaji wa masoko duniani.

Naibu Waziri Mkuu, Ahmad Zahid Hamidi, ametoa wito huo katika ufunguzi wa Maonesho ya 22 ya Kimataifa ya Halal Malaysia (MIHAS 2026) na Mkutano wa Kimataifa wa Halal mjini Kuala Lumpur.

Amesema kupata cheti cha halal pekee hakutoshi kuiwezesha kampuni kushindana kimataifa. Biashara pia zinahitaji uzalishaji wenye viwango thabiti, vifungashio vinavyofaa, mtaji, usafirishaji wa uhakika na uelewa wa masoko yanayolengwa.

Kwa sasa, ni asilimia 14.7 pekee ya kampuni zenye vyeti vya halal nchini Malaysia zinazouza bidhaa nje ya nchi.

Waziri wa Masuala ya Dini, Zulkifli Hasan, amesema uchumi wa halal unapaswa kujengwa juu ya misingi ya Sharia, uadilifu, maadili na uwajibikaji.

Malaysia inalenga kuimarisha nafasi yake katika soko la halal duniani kupitia viwango vinavyoaminika, ubunifu, teknolojia na ushirikiano wa kimataifa.

Kuporomoka kwa sarafu kwaongeza mateso Sudan

OMDURMAN, Sudan, Kuporomoka kwa thamani ya pauni ya Sudan kumeongeza ugumu wa maisha kwa wananchi wanaojaribu kujijenga upya baada ya zaidi ya miaka mitatu ya vita.

Kwa mujibu wa Reuters, pauni ya Sudan imepoteza karibu nusu ya thamani yake katika maeneo yanayodhibitiwa na jeshi tangu mwanzoni mwa majira ya kiangazi. Katika soko lisilo rasmi, dola moja imefikia takribani pauni 7,500, kutoka 4,100 mwezi Mei.

Kuporomoka huko kumesababisha bei za bidhaa muhimu kupanda huku uwezo wa wananchi kununua ukishuka.

Aisha Younis, aliyekuwa mwalimu, amesema lita moja ya mafuta ya kupikia ilipanda kutoka pauni 17,000 hadi 23,000 ndani ya wiki moja. Wafanyabiashara Omdurman wamesema mauzo yamepungua hadi asilimia 70.

Almutasim Abdulrahim, anayeendesha shule binafsi, amesema mshahara wake wa pauni 500,000 kwa mwezi ulikuwa sawa na dola 800 kabla ya vita, lakini sasa ni karibu dola 70. Hali hiyo imemlazimisha kufanya kazi ya ziada ya udereva ili kukidhi mahitaji ya maisha.

Kuwait yapitisha sheria ya kwanza ya Sukuk za serikali

KUWAIT CITY, Kuwait, Kuwait imepitisha sheria yake ya kwanza inayosimamia utoaji wa sukuk za serikali, hatua inayopanua njia za serikali kupata fedha kwa kutumia vyombo vinavyoendana na Sharia.

Kwa mujibu wa tovuti ya AGBI, sheria hiyo inaruhusu serikali kutoa sukuk kwa dinari ya Kuwait na sarafu za kigeni kupitia taasisi maalumu itakayofadhiliwa na Mfuko Mkuu wa Akiba wa Serikali.

Waziri wa Fedha wa Kuwait, Yacoub Al-Rifai, amesema sheria hiyo ni hatua muhimu katika kuendeleza mfumo wa ufadhili wa serikali kwa kuongeza aina za vyombo vinavyopatikana, ikiwemo sukuk zinazofuata misingi ya Sharia.

Mkuu wa Kituo cha Uchumi cha Al-Manakh, Ali Al-Anzi, amesema sheria hiyo pia inaweza kuchochea soko la madeni na kuongeza ushiriki wa benki za Kiislamu. Kuwait ina benki nne zinazofuata Sharia, zikiwemo Kuwait Finance House, Kuwait International Bank, Boubyan Bank na Warba Bank.

Hatua hiyo imekuja wakati mapato ya mafuta yakishuka na serikali ikiongeza ukopaji. Deni la umma lilifikia dinari bilioni 8.6, sawa na dola bilioni 28, mwishoni mwa Juni 2026.

Malaysia, Indonesia zaunda baraza la halal

KUALA LUMPUR, Malaysia, Malaysia na Indonesia zimeanzisha Baraza la Halal la pamoja kwa lengo la kuimarisha ushirikiano na kurahisisha biashara ya bidhaa halal kati ya nchi hizo mbili.

Kwa mujibu wa New Straits Times, ikinukuu Shirika la Habari la Bernama, Naibu Waziri Mkuu wa Malaysia, Ahmad Zahid Hamidi, amesema baraza hilo litaongozwa na Shirika la Indonesia la Usimamizi wa Uhakikisho wa Bidhaa Halal (BPJPH), huku Malaysia ikishika nafasi ya Katibu Mkuu.

Mkutano wa kwanza wa baraza hilo unatarajiwa kufanyika Oktoba, ukilenga kurahisisha utambuzi wa vyeti vya halal na kupunguza urudiaji wa taratibu za biashara.

NA UKHTI FATIMA

Zingatia haya kujilinda dhidi ya utapeli mitandaoni

Utapeli wa mtandaoni hauhitaji kila mara tapeli avunje mfumo wa benki au awe bingwa wa kompyuta. Mara nyingi anachohitaji ni kukufanya uamini, uogope, uwe na tamaa au ufanye haraka.

Ndiyo maana kinga bora si kujua kila aina mpya ya utapeli. Mbinu hubadilika kila siku. Muhimu ni kuelewa wanavyotutapeli na kuwa na kanuni ambazo hatuzivunji hata tunapobanwa na mazingira.

Wanatutapeliaje?

Mbinu kubwa ni ujanja wa kisaikolojia. Tapeli anakushawishi wewe mwenyewe umfungulie mlango.

Anaweza kupiga simu akijifanya mfanyakazi wa benki, kampuni ya simu, polisi au taasisi ya serikali. Atadai akaunti yako imefungwa, kuna muamala wa kutia shaka au tatizo linalohitaji kutatuliwa haraka. Kisha ataomba namba yako ya siri, nenosiri au namba ya uthibitisho ya matumizi ya mara moja.

Mwingine atakutumia ujumbe unaofanana na taarifa ya kutumiwa fedha kwa simu, kisha akupigie akisema ametuma kimakosa. Ukirudisha bila kuangalia salio lako halisi, unaweza kuwa umetuma fedha zako mwenyewe.

Kuna pia ughushi wa utambulisho wa kidijitali. Namba ya simu inaweza kuonekana kama ya taasisi unayoijua. Barua pepe inaweza kufanana na ya kampuni halali. Tovuti inaweza kufanana kabisa na ya benki, huku tofauti ikiwa herufi moja tu katika anuani.

Kwa hiyo, nembo nzuri, picha rasmi au namba inayoonekana sahihi si uthibitisho wa uhalali.

Mitandao ya kijamii nayo ni eneo kubwa la utapeli. Tapeli anaweza kufungua ukurasa mzuri wa Instagram au Facebook, kuweka picha za simu, nguo, vipuri au vifaa vingine kwa bei ya kuvutia na kuomba malipo kabla ya bidhaa kutumwa. Baada ya kulipa, anakuzuia au ukurasa unatoweka.

Wengine hutumia ajira, mikopo, viza, zabuni au uwekezaji wa uongo. Unaambiwa ulipe "ada ya usajili," "gharama za mchakato" au "amana" kabla ya kupata kazi, mkopo au faida kubwa. Ahadi ya fedha nyingi kwa haraka na bila hatari ni ishara kubwa ya tahadhari.

Kuna pia hadaa ya kunasa taarifa binafsi. Unapokea barua pepe, ujumbe mfupi au ujumbe wa WhatsApp wenye kiunganishi. Ukikibofya, unaingia kwenye tovuti bandia inayofanana na ya taasisi halali. Ukiandika nenosiri, taarifa za benki au namba ya uthibitisho, unamkabidhi tapeli funguo za akaunti yako.

Wengine hujenga urafiki au uhusiano wa kimapenzi kwa wiki au miezi, kisha huanza kuomba fedha kwa madai ya matibabu, safari, mzigo uliokwama au dharura nyingine.

Hatari nyingine ni kuombwa kusakinisha programu ili mtu "akusaidie" kurekebisha simu au kompyuta. Programu hiyo inaweza kumpa uwezo wa kuona skrini yako, kuingia kwenye akaunti au kuiba taarifa zako.

Na ukishatapeliwa, unaweza kutapeliwa tena. Tapeli mwingine anaweza kujitokeza akidai anaweza kurejesha fedha zako, lakini akataka kwanza "ada ya uchunguzi" au "gharama za kurejesha fedha."

Namna ya kujikinga

Kwanza: Tafakari kabla ya kutenda. Haraka ni silaha ya tapeli. Ukiambiwa "lipa sasa," "akaunti inafungwa," au "nafasi inaisha dakika chache," usifanye uamuzi hapohapo. Simama, fikiria na hakiki.

Pili: Hakiki kwa njia tofauti. Mtu akisema anatoka benki, kata simu na piga namba rasmi unayoijua. Rafiki akiomba fedha WhatsApp, mpigie moja kwa moja. Usitumie namba au kiunganishi alichokutumia mtu anayekushuku.

Tatu: Linda siri zako. Namba ya siri, nenosiri na namba ya uthibitisho ni zako. Usimpe mtu yeyote. Taasisi halali haihitaji siri hizo ili kukusaidia.

Nne: Usibofye viunganishi kwa mazoea. Ujumbe ukidai umetoka benki au taasisi, fungua mwenyewe programu rasmi au andika anuani ya tovuti. Angalia tahajia kwa makini; tapeli anaweza kubadilisha herufi moja na kutengeneza tovuti bandia.

Tano: Tumia manenosiri tofauti. Nenosiri moja likiibiwa lisifungue akaunti zako zote. Tumia manenosiri marefu, magumu kutabirika na, inapowezekana, uthibitishaji wa hatua mbili au zaidi.

Sita: Usimruhusu mtu usiyemjua kuingia kwenye simu au kompyuta yako akiwa mbali. Ukihitaji msaada wa kiufundi, tumia mtoa huduma unayemwamini.

Saba: Chunguza kabla ya kulipa. Bei ikiwa nzuri kupita kawaida, ongeza tahadhari. Tafuta historia ya muuzaji, anwani, maoni ya wateja na taarifa za usajili. Wafuasi wengi au picha nzuri si uthibitisho wa uhalali.

Nane: Kuwa mwangalifu na malipo ya awali. Ajira, zawadi, mikopo, mirathi au fursa nyingine inayotaka ulipe kwanza inahitaji uchunguzi mkubwa.

Tisa: Linda taarifa zako binafsi. Tarehe ya kuzaliwa, anuani, picha, mahali pa kazi na taarifa za familia zinaweza kutumiwa kukulenga au kuiba utambulisho wako.

Kumi: Ukishatapeliwa, chukua hatua haraka. Wasiliana na benki au kampuni ya simu, badili manenosiri, zuia akaunti inapowezekana na hifadhi ushahidi. Tanzania, TCRA inaelekeza namba zinazohusishwa na utapeli kuripotiwa kwa kutuma neno UTAPELI kwenda 15040, huku makosa ya jinai yakiripotiwa Polisi.

Kanuni kuu ni hii: usiamini kwa sababu kitu kinaonekana halisi. Thibitisha kabla ya kubofya, kutoa taarifa au kutuma fedha.

NA
Na Abeid Othman
0754 990 083

Athari umma unaposhindwa kupanga na kuchagua vema vipaumbele

Tanzania ina idadi kubwa ya Waislamu ambao, kama ilivyo kwa jamii nyingine, wanakabiliwa na changamoto mbalimbali katika maisha yao ya kila siku. Changamoto hizo zinagusa elimu, afya, uchumi, ajira, ujuzi wa kitaalamu, malezi, huduma za kijamii, maendeleo ya vijana na hata ustawi wa familia.

Athari umma unaposhindwa kupanga na kuchagua vema vipaumbele

Tanzania ina idadi kubwa ya Waislamu ambao, kama ilivyo kwa jamii nyingine, wanakabiliwa na changamoto mbalimbali katika maisha yao ya kila siku.

Changamoto hizo zinagusa elimu, afya, uchumi, ajira, ujuzi wa kitaalamu, malezi, huduma za kijamii, maendeleo ya vijana na hata ustawi wa familia.

Hata hivyo, pamoja na ukubwa wa changamoto hizi, tatizo jingine kubwa linalotukabili ni kushindwa kama umma kujua tunataka kuchagua nini, kuweka vipaumbele gani na kupanga mikakati ya pamoja ya kukabiliana na matatizo hayo.

Tatizo si kwamba hakuna watu wanaofanya kazi. Tatizo ni kwamba mara nyingi tunafanya kazi bila dira ya pamoja.

Kuna taasisi, mashirika, misikiti, vikundi na watu binafsi wanaofanya juhudi kubwa katika maeneo mbalimbali. Lakini juhudi hizo wakati mwingine hazijaunganishwa na mpango mpana unaoeleza tunataka kufikia nini? Ni changamoto zipi tunapaswa kuanza nazo? Nani afanye nini na kwa muda gani?

Hatuna vipaumbele

Umma wa Kiislamu Tanzania una matatizo katika karibu kila sekta. Tunahitaji kuongeza ubora na upatikanaji wa elimu kwa watoto wetu wote, huduma bora za afya kwa bei inayohimilika na zinazozingatia misingi ya sharia, nafasi zaidi za ajira, ujasiriamali na mitaji kwa vijana sambamba na mafunzo ya ujuzi na mazingira yatakayowawezesha kujitegemea.

Tunahitaji pia huduma kwa makundi mahsusi ikiwemo watoto, wanawake, wazee na watu wenye mahitaji mbalimbali.

Lakini tunapokabiliwa na matatizo mengi kwa wakati mmoja, si busara kujaribu kufanya kila kitu kwa wakati mmoja bila mpango. Tunahitaji kujifunza kuchagua.

Kuchagua hakumaanishi kuacha matatizo mengine bali inaamisha kutambua ni jambo gani lina athari kubwa zaidi, kulipa kipaumbele, kulitengenezea mpango, kulitafutia rasilimali na kulisimamia mpaka litokee. Baada ya hapo, tunahamia kwenye kipaumbele kingine.

Kwa mfano, kama tumekubaliana kwamba vijana ni nguvu kazi ya jamii, tunaweza kuamua kwa pamoja kuwekeza zaidi katika vyuo vya ufundi na vituo vya mafunzo ya teknolojia, biashara na ujuzi mbalimbali.

Kama tumeona afya ni changamoto kubwa, tunaweza kupanga kujenga zahanati, vituo vya afya na hospitali katika maeneo yenye uhitaji. Kama elimu ya juu ni kipaumbele, tunaweza kuweka nguvu katika kuanzisha na kuimarisha vyuo vikuu na taasisi za kitaalamu.

Huo ndio upangaji wa kimkakati; si kufanya kila kitu kwa wakati mmoja, bali kuchagua kwa busara kile tunachoweza kufanya vizuri.

Taasisi zibadilike

Moja ya matokeo ya kukosa mpango wa pamoja ni kuwa na taasisi nyingi zikifanya programu zinazofanana bila uratibu wa kutosha. Taasisi moja inaweza kuanzisha mradi fulani, nyingine ikaona huo ndio mradi unaofaa na kuanzisha kitu kinachofanana, huku eneo jingine lenye uhitaji mkubwa likibaki bila huduma.

Ushindani wa namna hii haujengi umoja wa maendeleo.

Ni vizuri taasisi mbalimbali kufanya kazi, lakini tunahitaji pia mgawanyo wa majukumu na uratibu. Kama taasisi moja ina uwezo mkubwa katika elimu, iwekeze zaidi huko. Nyingine ikiwa na uwezo katika afya, iwekeze katika afya. Nyingine ikiwa na uwezo wa kiuchumi, iandae programu za ajira, ujasiriamali na uwezeshaji. Kwa kufanya hivyo, nguvu ndogo ndogo zinaweza kugeuka kuwa nguvu kubwa ya pamoja.

Tatizo kubwa zaidi linatokea pale ambapo baadhi yetu, badala ya kuangalia matokeo ya kazi, tunaanza kuwakosoa wanaofanya jambo fulani kwa sababu za kimadhehebu au manhaj. Mtu akifanya jambo ambalo sisi hatulifanyi, badala ya kujiuliza kwa nini sisi tusifanye jambo jema kama hilo, tunaanza kutafuta sababu za kulikosoa.

Hii inatufanya tupoteze muda na nguvu. Ikiwa taasisi fulani imeanzisha chuo cha ufundi na kinasaidia vijana kupata ujuzi, taasisi nyingine haipaswi kutumia nguvu nyingi kusema kwa nini wao wameanzisha chuo hicho.

Badala yake, inaweza kusema: “Hili ni jambo jema; sisi tunaweza kufanya nini zaidi?”

Tunahitaji kujifunza kushindana kwa kufanya vizuri zaidi, si kushindana kwa kuonyesha makosa ya wengine.

Kunyoosheana vidole kuwe mwiko

Mahitaji ya Waislamu wa Tanzania leo yanahitaji fikra pana na mipango inayotazama miaka mingi ijayo katika elimu, afya, ajira, uchumi kwa ujumla. Hayo yote hayawezi kufanyika kwa malumbano na ruduud za majukwaani. Yanahitaji mipango, fedha, wataalamu, uongozi, uwajibikaji na uvumilivu.

Ni wakati wa kujiuliza maswali magumu: Tunataka Waislamu wa Tanzania wawe katika hali gani baada ya miaka 10, 20 au 100 ijayo? Ni taasisi zipi tunahitaji? Ni wataalamu wangapi tunahitaji kuzalisha? Ni maeneo gani yanahitaji hospitali?

Ni vijana wangapi wanahitaji mafunzo ya ufundi? Ni mikakati gani inaweza kuongeza uwezo wetu wa kiuchumi?

Tukianza kuulizana maswali haya, tutaanza kutoka katika siasa za lawama na kuingia katika siasa za suluhisho.

Ujue Waqf wa dharura na majanga

Katika uelewa wa kawaida, Waqf huhusishwa zaidi na kujenga misikiti na madrasa, kuchimba visima, au kutenga mali kwa ajili ya huduma za muda mrefu za jamii. Hata hivyo, historia na Fiqhi ya Kiislamu vinaonesha uwezekano wa kutumia mali ya Waqf kama nyenzo ya kukabiliana na dharura na majanga kama; mafuriko, ukame, njaa, milipuko ya magonjwa na majanga mengine yanayotishia maisha na ustawi wa jamii. Dhana hii inaweza kuitwa Waqf at-Twawari-i, yaani Waqf wa Dharura.

Msingi mkuu wa Waqf at-Twawari-i unatokana na malengo ya Sharia (Maqaswidu as-Shariah), hasa kulinda uhai na kuondoa madhara. Uislamu unahimiza kusaidiana katika mema na kuharakisha kuwanusuru wenye mahitaji.

Mwenyezi Mungu anasema: "Basi shindaneni katika kufanya kheri." [Qur'an, 2:148]. Aidha, anasema: "Na katika hayo, washindane wenye kushindana." [Qur'an, 83:26].

Kwa msingi wa kanuni za kuondoa madhara na kutanguliza maslahi ya msingi ya binadamu, mali za Waqf zinaweza kuwa sehemu ya mfumo wa maandalizi na mwitikio wa majanga. Hata hivyo, matumizi ya mali ya Waqf yanapaswa kuzingatia masharti ya wakif (mtoa Waqf), aina ya Waqf , maslahi ya Waqf u na hukumu za Fiqhi.

Kubadilisha matumizi ya mali ya Waqf (ibdal al-Waqf) au kubadilisha matumizi kwa maslahi ya msingi) si jambo la kufanywa kiholela, bali linahitaji msingi wa Kisharia na usimamizi wa mamlaka husika.

Historia ya Waislamu pia inatoa mifano ya namna rasilimali za jamii zilivyotumika wakati wa majanga. Katika Mwaka wa Ramadi, wakati wa ukame na njaa katika zama za Khalifa Umar ibn al-Khattwab (Allah amridhie), serikali na taasisi za jamii ziliandaa msaada wa chakula na mahitaji ya msingi kwa waathirika.

Katika Dola ya Ottoman pia kulikuwepo Waqf zilizolenga kusaidia watu waliokumbwa na majanga, ikiwemo moto na mafuriko, kwa kuwapatia mahitaji kama chakula, mavazi na malazi.

Katika zama hizi, dhana hii inaweza kutumika kwa mfumo mpana zaidi. Cash Waqf inaweza kuanzishwa kama mfuko maalumu wa dharura unaoweza kusaidia ununuzi wa vifaa vya afya, chakula, maji, malazi na mahitaji mengine muhimu wakati wa janga.

Wakati wa COVID-19, taasisi mbalimbali za Kiislamu zilitumia au kuelekeza rasilimali za misaada na Waqf katika kusaidia huduma za afya na watu waliopoteza vipato. Vilevile, Waqf unaweza kuunganishwa na Qardhun Hasan (mkopo nafuu na mwema) ili kusaidia kaya na wafanyabiashara wadogo kurejesha shughuli zao baada ya janga bila kuingia katika mikopo yenye riba.

Kwa Tanzania, mfumo huu unaweza kuwa sehemu ya Waqf wa Kimkakati wa Taifa, kwa kuanzisha mfuko maalumu wa dharura wenye taratibu zilizo wazi za ukusanyaji, uwekezaji, utoaji na uwajibikaji.

Mfuko huo unaweza kuandaliwa kabla ya janga kutokea ili uweze kuitikia kwa haraka majanga kama mafuriko, ukame, magonjwa ya mlipuko, njaa au athari za mabadiliko ya tabianchi.

Hivyo, Waqf haupaswi kuonekana kama chombo cha kujenga miundombinu pekee. Ukiandaliwa kwa misingi sahihi ya Sharia na kusimamiwa kwa amana, weledi, uwazi na uwajibikaji, unaweza kuwa kinga ya kijamii inayosaidia kuokoa maisha, kupunguza madhara na kuijenga jamii yenye uwezo wa kustahimili majanga.

Na Said Rajab

0783 650 803

Milango muhimu ya bahari na hatma ya uchumi wa dunia

SEHEMU YA MWISHO 2

Katika sehemu ya kwanza ya makala haya wiki iliyopita, tulijadili umuhimu wa milango ya bahari katika uchumi wa dunia na biashara ya kimataifa. Tulieleza kwamba vita halisi havihusu milango hiyo pekee, bali pia wale wanaosimamia usalama wake na wenye uwezo wa kudhibiti njia zinazotumika katika usafirishaji wa biashara ya kimataifa. Sasa tuhitimishe sehemu ya mwisho ya makala haya.

Mlango–Bahari wa Hormuz haupaswi kutazamwa kama eneo la kijiografia lililotengwa, bali kama sehemu ya mapambano mapana ya ushawishi, nishati, biashara na usalama.

Iran inalenga kudumisha uwezo wake wa kijeshi ili kubaki na ushawishi katika mapambano yake na Marekani. China, kwa upande wake, inahitaji njia salama na thabiti za biashara na nishati, huku Ulaya ikitaka kuzuia usambazaji wa nishati na njia za baharini kutumiwa kama zana za vitisho vya kisiasa.

Marekani nayo inalenga kudumisha nafasi yake kama mhimili muhimu wa usalama katika Mashariki ya Kati. Kwa hiyo, kurejea kwa hali ya kawaida katika Mlango–Bahari wa Hormuz huenda isiwe mwisho wa mgogoro wa muda mfupi, bali ikawa sehemu ya mpango mpana zaidi.

Katika hali hiyo, urambazaji unaweza kurejea katika hali yake ya kawaida na biashara ya kimataifa ikaendelea kutiririka, lakini chini ya mifumo mipya ya usalama itakayoainisha nani ana uwezo wa kushawishi na kudhibiti njia hii muhimu ya bahari.

Hapa ndipo tunapokutana na kitendawili kingine: biashara ya kimataifa inahitaji milango ya bahari iwe wazi kwa wote, lakini Marekani inatafuta kudumisha uwezo mkubwa wa kushawishi usalama na uendeshaji wa njia hizo.

Katika mzozo huu, Mlango–Bahari wa Hormuz si tu njia ya maji inayotenganisha Iran na eneo la Ghuba, bali pia unazidi kuwa kitovu cha majadiliano ya kimataifa kuhusu mustakabali wa nishati, biashara na ushawishi.

Yeyote anayesimamia usalama wa njia hizi za bahari huwa na uwezo mkubwa wa kushawishi mtiririko wa biashara ya kimataifa. Hatua hii ni muhimu hasa katika dunia ya sasa, ambapo nishati imefungamana kwa karibu na uchumi, siasa na usalama, hali inayoufanya Mlango–Bahari wa Hormuz kuwa eneo muhimu kimkakati..

NA YUSUFU AMINI

Watoto kutelekeza wazazi, tatizo liko hapa

Katika jumla ya mambo mema ya kiibada ambayo jamii yetu imeyarithi kutoka vizazi vilivyopita ni kuwaheshimu na kuwahudumia wazazi (baba na mama). Hata hivyo, inasikitisha kusikia kwamba katika nchi yetu wapo watu wanaowanyanyapaa wazazi wao na kutoonyesha utu na heshima kwao.

Kauli tunazozisikia mara kwa mara kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kwamba baadhi ya wazazi wametelekezwa na watoto wao zinatufanya tujiulize: Watanzania sisi, ambao kwa miaka mingi tumesifika kwa kuwaheshimu wazazi, tunaelekea wapi? Hili ni swali ambalo kila mmoja wetu anapaswa kujiuliza na kuchukua hatua za kurekebisha hali hii kabla haijafikia pabaya.

Kwanza, sote tuelewe kuwa kuwaheshimu na kuwahudumia wazazi wetu si jambo la hiari wala tendo la ziada la wema, bali ni wajibu wa kidini unaopaswa kutekelezwa kwa upendo na heshima, kadiri ya uwezo wetu.

Heshima hiyo inapaswa kudhihirika katika maneno, matendo na namna tunavyowahudumia.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: "Na Mola wako ameamuru kwamba: Msimuabudu yeyote isipokuwa Yeye Pekee na muwafanyie wema wazazi wawili. Kama mmoja wao akifikia uzee naye yuko pamoja nawe, au wote wawili, basi usiwaambie, 'Ah!' Wala usiwakemee, na sema nao kwa maneno ya heshima. Na wainamishie bawa la unyenyekevu kwa huruma, na useme: Mola wangu! Warehemu kama walivyonilea nilipokuwa mdogo." ***[Qur'an 17:23–24].***

Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) pia amesisitiza kwa nguvu wajibu huo, akieleza kuwa kuwafanyia wema wazazi ni miongoni mwa ibada zenye daraja kubwa mbele ya Allah.

Imepokewa hadith kutoka kwa Abdullah bin Mas'ud (Allah amridhie) kwamba alimuuliza Mtume (Allah amshushie rehema na amani): "Ni amali gani inayopendwa zaidi na Allah?" Mtume akajibu: "Kuswali kwa wakati wake."

Ibn Mas'ud akauliza: "Kisha ipi?" Mtume akamjibu: "Kuwafanyia wema wazazi wawili." Akauliza tena: "Kisha ipi?" Mtume akajibu: "Jihad katika njia ya Allah." [Bukhari na Muslim].

Katika tukio jingine, mtu mmoja alimwendea Mtume (Allah amshushie rehema na amani) akiomba ruhusa ya kwenda katika Jihad. Mtume akamuuliza kama wazazi wake wangali hai. Baada ya kuthibitisha kuwa wazazi wake wangali hai, Mtume akamuamuru aelekeze juhudi zake katika kuwahudumia.

Ujumbe huu una maana kubwa katika jamii ya leo. Mtoto anayewahudumia wazazi wake hafanyi tu tendo la huruma, bali anatekeleza jukumu lililowekwa na dini. Kuwahudumia wazazi ni sehemu ya ibada, na kuwatelekeza ni jambo ovu linaloweza kumuingiza mtu Motoni.

Mtume amesema: "Amepata hasara, amepata hasara, amepata hasara yule aliyewadiriki wazazi wake wawili au mmoja wao hadi wakazeeka, kisha asiingie Peponi (kwa sababu ya kutowafanyia wema)." [Muslim].

Kwa msingi huo, hata tendo dogo linaloashiria kukerwa linaweza kwenda kinyume na adabu ambayo Uislamu umewawekea watoto katika kuwatunza wazazi wao.

Kadiri mzazi anavyozeeka, ndivyo mtoto anavyopaswa kuongeza huruma, msaada, subira na heshima kwake. Kuhudumia wazazi ni njia ya karibu zaidi ya kupata radhi za Allah na kuingia Peponi. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Mzazi ndiyo mlango bora miongoni mwa milango ya Peponi; ukitaka unaweza kuupoteza au kuuhifadhi." [Tirmidhi].

Kwa hiyo, kuwadharau, kuwapuuza au kuwanyanyasa wazazi kunaweza kumnyima mtu fursa ya kupata radhi za Allah na hatimaye kumzuia kuingia Peponi. Pamoja na hayo, tunapaswa kukumbuka kuwa namna tunavyowatendea wazazi wetu leo, ndivyo nasi tutakavyotendewa siku tutakapofikia uzee.

Kiini cha tatizo

Kuunda sheria ya kuwalazimisha watoto kuwatunza na kuwahudumia wazazi wao, kama baadhi ya watu wanavyopendekeza, ni ishara kwamba jamii haielewi tatizo liko wapi. Katika Uislamu, kuwaheshimu, kuwajali na kuwahudumia wazazi si wajibu unaotekelezwa kwa hofu ya sheria za nchi, bali ni sehemu ya msingi ya maadili na ibada.

Kwa hiyo, kabla ya kufikiria kuunda sheria, jamii inapaswa kujiuliza kwa nini malezi ya familia yamefikia hatua ambayo mtoto anahitaji kulazimishwa kutekeleza jambo ambalo dini yake tayari imemfundisha kuwa ni wajibu.

RABIU UL THANI 18, 1448

VISION 2050

ربيع ثان

SAFARI YA MABADILIKO

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

ELIMU YA MAZISHI YA KIISLAMU

Je, mila hizi katika mazishi ni sehemu ya Uislamu?

SEHEMU YA

7

Mtu anapofiwa, mara nyingi hukutana na ushauri mwingi kutoka kwa ndugu, marafiki na majirani. Wapo watakaosema: "Lazima mfanye hivi." Wengine watasema: "Kwetu tumekuwa tukifanya hivi tangu zamani." Na wengine watasisitiza: "Msipofanya jambo fulani, si vizuri kwa marehemu."

Lakini swali muhimu ni hili: Je, kila jambo lililozoeleka katika mazishi ni sehemu ya Uislamu? Jibu ni hapana. Dini imejengwa juu ya wahyi. Allah Mtukufu amesema: "Leo nimekukamilishieni dini yenu, nimekutimizieni neema Yangu juu yenu, na nimekupendeleeni Uislamu uwe dini yenu." [Qur'an, 5: 3].

Aya hii inaonesha kwamba dini ilikamilika wakati wa Mtume (Allah amshushie rehema na amani). Hivyo, hakuna ibada inayoweza kuongezwa baada ya kukamilika kwa dini isipokuwa kwa dalili kutoka katika Qur'an au Sunna.

Mazishi ni ibada

Baadhi ya watu hudhani kwamba mazishi ni jambo la kijamii tu, hivyo kila wanaweza kuongeza au kupunguza jambo lolote kadri wanavyotaka.

Lakini ukweli ni kwamba kuosha maiti ni ibada; kumvika sanda ni ibada; Swala ya

Janaza ni ibada; kuzika ni ibada; hata dua za baada ya mazishi zimefundishwa. Kwa hiyo, ibada hizi haziwezi kubadilishwa kwa kufuata hisia, utashi au tamaduni wa mtu.

Mila si kigezo cha hukumu

Uislamu haukatazi mila zote. Kanuni ni kwamba mila zinazokubalika na Sharia zinaweza kuendelea. Lakini mila inayopingana na Qur'an au Sunna sahihi haiwi sahihi kwa sababu tu imekuwepo kwa muda mrefu au mbona kwa hoja kwamba fulani anafanya.

Imam Malik (Allah amrehemu) alisema: "Mambo ya mwisho ya Umma huu hayawezi kuwa mazuri isipokuwa kwa yale yaliyoyafanya mambo ya mwanzo wake kuwa mazuri."

Yaani, suluhisho la kurekebisha jamii ni kurejea kwenye Qur'an na Sunna.

Hatari ya kuifanya mila kuwa dini

Tatizo kubwa hutokea pale ambapo desturi hupewa uzito sawa na ibada. Mfano: Mtu akiacha Sunna, hakuna anayemkemea.

Lakini akiacha desturi fulani ya kijamii, huwa nongwa na huonekana amefanya kosa kubwa. Hapo ndipo mila huwa imechukua nafasi ya dini na hili ndilo ambalo wanazuoni walikuwa wakilihofia.

Tuyapime mambo kwa mizani gani?

Muislamu anapaswa kujiuliza maswali manne: Kwanza: Je, jambo hili lina dalili sahihi kutoka kwenye Qur'an au Sunna? Pili: Je, Mtume (Allah amshushie rehema na amani) au Swahaba walilifanya? Tatu: Je, wanazuoni wa mwanzo wa Umma walilifahamu na kulikubali? Nne: Je, linaendana na makusudio ya Sharia?

Maswali haya humsaidia Muislamu kutofautisha kati ya Sunna na mazoea ya watu.

Tusikimbilie Kuhukumu

Pamoja na hayo, ni muhimu kuwa na hekima. Si kila anayefanya jambo lisilo na dalili analifanya kwa makusudi. Wengi walelikuta kutoka kwa wazazi wao au jamii zao.

Kwa hiyo, wajibu wa wenye elimu ni kufundisha kwa upole, si kuwavunjia heshima watu au kuwagawa Waislamu.

Allah anasema: "Lingania katika njia ya Mola wako Mlezi kwa hekima na mawaidha mazuri." [Qur'an, 16: 125]..

Tunajifunza nini?

Katika mfululizo huu, tutakuwa tukirejea mara kwa mara kwenye kanuni hii: Mazishi ya Kiislamu ni ibada. Na kila ibada hufuata dalili; haifuati hisia; na wala haifuati shinikizo la jamii; haifuati mila zinazopingana na Sunna.

Hii ndiyo njia salama ya kumheshimu marehemu na kutekeleza haki yake.

Hitimisho

Muislamu hapaswi kuuliza: "Watu wetu wamezoea kufanya nini?" Bali aulize: "Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alitufundisha nini?" Maswali hayo mawili yanaweza kuonekana yanafanana, lakini majibu yake yanaweza kuwa tofauti kabisa.

Tutakapomfanya Mtume (Allah amshushie rehema na amani) kuwa kigezo chetu, tutahifadhi usafi wa ibada na tutakuwa tumewatendea haki waliotutangulia. Makala ijayo InshaaAllah: "Sanda ya Muislamu: Namna ya kumvika marehemu kwa mujibu wa Sunna."

Na Said Rajab

0783 650 803

Kujali ndugu kunavyodumisha mshikamano wa familia

SEHEMU YA 2

Katika toleo lililopita tuliishia na aya isemayo: "Na wala wasiape wale wenye fadhila miongoni mwenu na wenye wasaa wa mali kuwa hawatowapa (sadaka) jamaa wa karibu, na masikini, na Muhajirin katika njia ya Allah. Na wasamehe na waachilie mbali. Je, nyinyi hampendi Allah akusameheni? Na Allah ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu." [Qur'an, 24:22].

Tulisema kuwa aya hii inamuongoza Muislamu kuitikia makosa anayofanyiwa na ndugu zake kwa msamaha. Aidha, inamkumbusha kwamba yeyote anayetarajia msamaha wa Allah, naye anapaswa kuwasamehe waja wake. Sasa endelea na sehemu inayofuata.

Kipengele kimojawapo cha kuwatendea wema ndugu na jamaa ni kutafsiri maneno yao kwa mtazamo mzuri; yaani kuepuka kutafuta makosa yao, kuwashutumu au kusambaza kasoro zao.

Iwapo ndugu au jamaa anahitaji ushauri, basi unapaswa kutolewa kwa upole na kwa faragha, si kwa kumfedhehesha au kumtia aibu mbele ya jamii. Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) amesema: "Mwenye kuficha makosa ya ndugu yake Muislamu, Mwenyezi Mungu atamfichia makosa yake duniani na Akhera." [Bukhari].

Aina nyingine ya kuwatendea wema ndugu na jamaa ni kuzuia hasira na ghadhabu wakati wa ugomvi. Moja ya mambo muhimu zaidi katika kushughulika na ndugu ni kujizuia, kwa sababu ndugu au jamaa anaweza kuona kwa mwenzake mambo ambayo watu wengine hawawezi kuyaona.

Aidha, ugomvi baina ya wanafamilia unaweza kuwa mchungu zaidi na kudumu kwa muda mrefu. Kwa sababu hiyo, Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) amesema: "Mwenye nguvu si yule anayeweza kuwashinda wengine, bali ni yule anayejidhibiti anapokasirika." [Bukhari na Muslim].

Nguvu ya kweli haipo kwenye kupaza sauti, kumshinda mpinzani, au kujibu tusi kwa tusi lingine, bali ipo katika kuzuia hasira, kudumisha tabia njema na kuchelewesha majibu hadi hasira zitakapopoa.

Ni busara zaidi kuepuka kubishana unapokuwa na hasira. Chagua maneno mazuri na kumbuka kwamba kudumisha uhusiano wa kifamilia ni muhimu zaidi kuliko kushinda mabishano au kushikilia jambo linalopita.

Miongoni mwa njia za kuonesha wema kwa ndugu na jamaa ni kuwajali na kuwasaidia wenye mahitaji, wakiwamo masikini na wagonjwa, na kushirikiana nao wanapokabiliwa na changamoto mbalimbali.

Msaada huo unaweza kutolewa kwa namna tofauti, ikiwamo kifedha, kimwili au kihisia, kulingana na mahitaji ya mhusika na uwezo wa anayetoa msaada.

Itaendelea wiki ijayo Insha Allah

Na Samrath Msuya
0789 201 383

Saa ya mwili: Kwa nini wengine huchangamka usiku, wengine asubuhi

KUNA watu saa 11 alfajiri macho yao yako wazi kabisa. Wanaweza kuamka, kuoga, kusoma, kufanya mazoezi na kuanza kazi bila shida. Lakini wengine saa hizo, wanahisi kama dunia imewaonea. Wanaweza kuamka tu kwa ajili ya sala, si kazi nyingine. Hawa, utakuta 'alarm' inalia mara tatu, wanazima, wanalala tena. Hata wakifika kazini saa mbili asubuhi, akili yao haijawa tayari kufanya kazi nzito.

Ajabu ni kwamba mtu huyo huyo ambaye saa mbili asubuhi anaonekana mzito, saa mbili usiku anaweza kuwa macho kabisa, mwenye mawazo mengi na uwezo mkubwa wa kufanya kazi.

Je, ni uvivu? Si lazima.

Sayansi ya usingizi inaonyesha kuwa miili yetu haitofautiani tu kwa kiasi cha usingizi tunachohitaji. Pia tunatofautiana katika muda ambao mwili kwa asili unapendelea kulala, kuamka na kufanya kazi vizuri zaidi.

Hali hiyo huitwa chronotype.

Kwa lugha rahisi, chronotype ni tabia ya ndani ya mwili inayokufanya uwe zaidi mtu wa asubuhi, mtu wa usiku, au uwe katikati ya makundi hayo mawili.

Saa ya ndani ya mwili

Mwili wa binadamu una mfumo wa takribani saa 24 unaosimamia wakati wa kulala na kuamka, pamoja na shughuli nyingine kama joto la mwili, homoni na baadhi ya michakato ya mwili. Mfumo huo huitwa circadian rhythm, yaani saa ya ndani ya mwili.

Chronotype inahusiana sana na saa hiyo, lakini maneno hayo hayamaanishi kitu kilekile.

Fikiria watu wawili wenye saa zinazofanya kazi vizuri, lakini moja imepangwa kuwasha kengele mapema kuliko nyingine. Hivyo ndivyo miili yetu ilivyo.

Mtu mmoja huanza kupata usingizi mapema jioni na kuamka mapema bila shida. Mwingine huchelewa kupata usingizi na mwili wake hufikia kiwango kikubwa cha umakini baadaye mchana au jioni.

Utafiti unaonyesha kuwa tofauti hizo zina sehemu ya kinasaba, ingawa umri, mwanga tunaoupata na mazingira yetu pia vinaweza kuwa na athari. Chronotype pia hubadilika kwa kiasi fulani katika maisha: watoto wengi huamka mapema zaidi, vijana huwa na mwelekeo wa kuchelewa kulala na kuamka, kisha ratiba huanza kurudi mapema kadiri umri unavyoongezeka.

Wewe ni mtu wa asubuhi au usiku?

Kisayansi, watu hawawezi kugawanywa katika makundi machache yenye mipaka mikali. Chronotype ni kama mstari mrefu.

Upande mmoja kuna watu wa asubuhi. Hawa huamka mapema kwa urahisi na mara nyingi huwa na nguvu na umakini mkubwa zaidi asubuhi. Upande mwingine kuna watu wa usiku. Hawa huamka kwa shida mapema, lakini nguvu na umakini wao huongezeka kadiri siku inavyoendelea.

Katikati kuna watu wengi ambao si wa asubuhi sana wala wa usiku sana. Hivyo, kujua chronotype yako hakuhitaji kwanza kipimo cha hospitali.

Jiulize: Kama kesho huna kazi, shule, miadi wala wajibu wa kuamka kusali, ungejisikia kulala saa ngapi? Ungeamka saa ngapi bila kulazimishwa? Ni wakati gani wa siku akili yako huwa makini zaidi? Majibu hayo yanaweza kukupa dalili.

Tatizo huanza maisha yanapopingana na mwili

Chronotype yenyewe si ugonjwa. Changamoto kubwa hutokea pale saa ya mwili wako inapogongana kila siku na ratiba ya maisha.

Mfano rahisi ni mtu wa usiku anayelala vizuri zaidi saa sita au saba usiku lakini anatakiwa kuamka saa 11 alfajiri kila siku kusali sala ya Alfajiri na kwenda kazini. Anaweza kujilazimisha kuamka. Lakini hilo halimaanishi mwili wake umebadilika.

Matokeo yake yanaweza kuwa mtu anatumia siku za kazi akiwa na deni la usingizi, halafu Jumamosi na Jumapili analala hadi mchana.

Wataalamu huita mgongano huu social jetlag — hali inayofanana kwa namna fulani na usumbufu unaompata msafiri anayevuka maeneo yenye tofauti kubwa za saa. Tofauti ni kwamba hapa hujasafiri kwenda nchi nyingine; ratiba ya jamii ndiyo inayopingana na saa yako ya mwili.

Ina maana gani kazini, shuleni?

Hapa sayansi hii inapata matumizi muhimu sana kwa wazazi na walimu. Katika ujana, chronotype kwa kawaida huelekea kuchelewa. Kijana anaweza kutopata usingizi mapema kama mtoto mdogo, lakini bado anatakiwa kuamka mapema kwenda shule.

Tuseme una kazi inayohitaji umakini mkubwa: kuandika ripoti, kufanya hesabu, kubuni wazo au kutatua tatizo. Kama wewe ni mtu wa asubuhi, huenda kazi hiyo ukafanya vizuri zaidi mapema.

Kazi ni ibada, ifanye kwa ufanisi

Imepokewa kutoka kwa Aswim bin Kulaib, kutoka kwa baba yake (Allah awaridhie wote) akisema: "Nilihudhuria pamoja na baba yangu mazishi ambayo Mjumbe wa Allah (rehema na amani zimshukie) alihudhuria. Wakati huo nilikuwa bado kijana, lakini nilikuwa na ufahamu. Jeneza lilipopelekwa makaburini, kaburi lilikuwa bado halijaandaliwa vizuri kwa ajili ya kumlaza maiti.

Mtume (rehema na amani zimshukie) akasema: 'Sawazisheni lahdi (mwanandani) ya maiti huyu.' Kauli hiyo iliwafanya baadhi ya watu kudhani kuwa kusawazisha mwanandani ni sehemu ya Sunna.

Mtume akawageukia na kusema: 'Jueni kwamba jambo hili halimnufaishi maiti wala halimdhuru. Lakini Allah anapenda mmoja wenu anapofanya jambo au kazi, aifanye kwa ubora na ukamilifu.'"

Katika riwaya nyingine imekuja: "Hakika Allah anapenda mmoja wenu anapofanya kazi yoyote, aifanye kwa ustadi na ukamilifu." [Imepokewa na Bayhaqi katika Shu'ab al–Iman].

Mafundisho ya tukio hili:

Uislamu ni dini inayohamasisha kufanya kazi kwa bidii, uaminifu na ubora. Kufanya kazi na kutafuta riziki ya halali ni sehemu

ya ibada, iwapo Muislamu atanuia kutosheleza mahitaji ya familia yake, kujiepusha na kuwaomba watu au kupata uwezo wa kumuabudu Allah na kufanya mema.

Kutoka kwa Ka'b bin Ujrah (Allah amridhie) amesema, mtu mmoja alipita mbele ya Mtume (rehema na amani zimshukie). Maswahaba walipoona nguvu na uchangamfu wake wakasema: "Ewe Mtume wa Allah! Laiti nguvu na uchangamfu wake ungekuwa katika njia ya Allah!"

Mtume akasema: "Ikiwa ametoka kwenda kutafuta riziki kwa ajili ya watoto wake wadogo, basi yuko katika njia ya Allah. Ikiwa amekwenda kutafuta riziki kwa ajili ya wazazi wake waliozeeka, basi yuko katika njia ya Allah. Ikiwa anajitafutia mwenyewe ili kuepuka kuwaomba watu, basi yuko katika njia ya Allah. Na ikiwa ametoka kwa lengo la kujionesha na kujifaharisha, basi yuko katika njia ya shetani." [Twabarani].

Maadili ya mfanyakazi Muislamu

Katika Uislamu, kufanya kazi huambatana na maadili ambayo kila mfanyakazi anapaswa kuyazingatia. Miongoni mwa maadili hayo ni:

Mosi, kujitegemea

Muislamu anapaswa kujitafutia riziki kwa njia halali na kuepuka kuwa tegemezi bila sababu ya msingi. Mtume amesema: "Ni bora mmoja wenu achukue kamba yake, aende akakusanye kuni, azibebe mgongoni mwake kisha aziuze; Allah alinde heshima yake, kuliko kuwaomba watu bila kujali kama watampa au watamnyima." [Bukhari na Ibn Majah].

Pia Mtume amesema: "Hakuna mtu aliyekula chakula bora kuliko kile kilichotokana na kazi ya mikono yake. Hakika Nabii wa Allah, Daudi (amani iwe juu yake) alikuwa akila kutokana na kazi ya mikono yake." [Bukhari].

Pili, nguvu na uaminifu

Allah anasema kuhusu Nabii Musa: "Hakika mtu bora wa kumuajiri ni yule mwenye nguvu na mwaminifu." [Qur'an, 28:26]. Kadhalika, Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) amesema: "Muumini mwenye nguvu ni bora na anapendwa zaidi na Allah kuliko muumini dhaifu, na katika wote wawili kuna kheri." [Muslim].

Hivyo, mfanyakazi anapaswa kutekeleza majukumu yake ipasavyo, huku akizingatia uaminifu katika kazi, matumizi ya muda na utunzaji wa mali alizokabidhiwa.

Tatu, ubora na ufanisi

Mfanyakazi Muislamu hapaswi kufanya kazi kwa mazoea au uzembe, bali kwa ustadi na ukamilifu. Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Hakika Allah anapenda mmoja wenu anapofanya kazi yoyote, aifanye kwa ustadi na ukamilifu." [Abu Ya'la].

Kwa hiyo, mfanyakazi Muislamu anapaswa kuwa mchapakazi, mwaminifu, mchamungu na anayetekeleza wajibu wake kwa bidii na ubora. Tukio la Mtume kuagiza lahdi (mwanandani) ya maiti isawazishwe linatukumbusha umuhimu wa kufanya kila jambo kwa umakini na ukamilifu.

Aidha, mfanyakazi anapaswa kuwa na nia njema, tabia nzuri na muamala mwema. Anapowahudumia wengine, awapokee kwa heshima, awasalimie, awasikilize na kuwaaga kwa maneno mazuri. Heshima, upole na ushirikiano vinapaswa kuwa sehemu ya utendaji wake wa kila siku.

Kupitia mafundisho haya ya Uislamu kuhusu maadili ya kazi, tunatambua kuwa kazi si njia ya kupata kipato pekee, bali pia ni dhamana na fursa ya kujenga jamii yenye uadilifu, uwajibikaji na ustawi.

Na Ukhti Fatima SS
0789 201 383

Mambo 6 yanayopeleka upotevu wa muda vikaoni

Kuna taasisi ambazo watu wanaweza kutumia saa mbili katika kikao, wakatoka wamechoka, lakini ukiwauliza: "Mmeamua nini?" jibu lisieleweke. Wiki inayofuata wanakutana tena kujadili yale yale.

Tatizo si kwamba vikao havina umuhimu. Vikao vinaweza kusaidia kutatua matatizo, kufanya maamuzi, kupata mawazo na kuratibu kazi. Tatizo ni namna vinavyoendeshwa.

Mark Murphy wa akiandika makala katika tovuti ya Leadership IQ anasema viongozi wengi wanapoulizwa kitu kinachopoteza muda na kupunguza tija kazini, jibu linalojitokeza mara nyingi ni vikao. Anabainisha matatizo sita yanayofanya vikao kuchukiwa—na namna ya kuyarekebisha.

Mosi, kikao ni kirefu kuliko kazi yake

Kuna tabia ya kupanga kikao cha saa moja kwa sababu kalenda imetenga saa moja. Matokeo yake, jambo ambalo lingeweza kumalizika kwa dakika 20 linavutwa mpaka saa iishe.

Suluhisho ni kuacha kupima kikao kwa muda na kukipima kwa matokeo. Kabla ya kuitisha kikao, kiongozi ajaze sentensi hii: "Baada ya kikao hiki tutakuwa tumefanikisha ______."

Kama huwezi kujaza nafasi hiyo kwa jambo mahususi, huenda kikao hakihitajiki.

Kama lengo limefikiwa baada ya dakika 25, kikao kiishe. Hakuna sababu ya kuendelea kuzungumza ili tu kutimiza saa.

Pili, watu wanachelewa

Kuchelewa kwenye kikao kunaonekana kosa dogo, lakini gharama yake ni kubwa. Watu wanane wakimsubiri mmoja kwa dakika 15, si dakika 15 tu zilizopotea; ni jumla ya muda wa watu wote waliokuwa wakisubiri.

Murphy anashauri taasisi ziachane na utamaduni wa kuwavumilia wanaochelewa. Kikao kianze kwa wakati. Aliyechelewa asifanye wengine warudie mjadala kwa ajili yake.

Ujumbe uwe wazi: muda wa kikao ni rasilimali ya taasisi.

Tatu, kikao hakizai chochote

Tatizo jingine ni kutumia dakika za mwanzo kwenye salamu ndefu, taarifa ndogo ndogo na mambo yasiyo muhimu, halafu hoja kubwa ikaletwa watu wakiwa wamechoka na muda umeisha.

Wakati ambao akili za watu bado ziko makini ndio unaopaswa kutumika kwenye jambo muhimu zaidi.

Ajenda nayo isiwe orodha ya maneno pekee. Kwa kila hoja ijulikane: tunajadili nini, kwa nini tunakijadili, tunataka kupata matokeo gani na washiriki wanapaswa kujiandaa vipi kabla ya kufika.

Kikao hakipaswi kuwa mahali pa watu kuja kuanza kufikiria. Waje wakiwa tayari kufikiri pamoja.

Nne, watu wasiostahili kuwapo wanaalikwa

Tumekuwa na desturi ya kuona ni bora kuwaalika watu wengi ili "wote washirikishwe." Lakini si kila mtu anayehusiana na taasisi anahitaji kukaa kwenye kila kikao.

Kabla ya kutuma mwaliko, jiulize: Mtu huyu ana taarifa, utaalamu, mamlaka au ushawishi unaohitajika ili kikao hiki kifikie matokeo? Kama jibu ni hapana, usimualike. Na hata anayehitajika kwenye hoja moja si lazima akae saa mbili kusubiri hoja yake. Anaweza kuingia wakati unaohitajika na kuondoka baada ya mchango wake.

Murphy anatumia kanuni ya kuchekesha lakini yenye ujumbe: kama watu wa kikao ni wengi kuliko wanaoweza kulishwa kwa pizza mbili, huenda kikao ni kikubwa kupita kiasi.

Tano, watu hawasikilizi

Katika baadhi ya vikao, mmoja anazungumza, mwingine yuko kwenye simu, mwingine anajibu ujumbe na mwingine amekaa kimya akisubiri kikao kiishe. Wakati mwingine tatizo si watu; ni namna kikao kinavyoendeshwa.

Waulize washiriki maswali yanayowalazimisha kufikiri: "Ni mazingira gani yanaweza kufanya uamuzi huu ushindwe?" "Tulikuwa na njia gani nyingine?" "Kama tungeanza kutoka mwanzo, tungechagua suluhisho hili?" Mtu anayetarajia kuombwa maoni ana sababu ya kufuatilia mjadala.

Sita, kikao kinaisha bila uwajibikaji

Hili huenda ndilo tatizo kubwa zaidi. Watu wamezungumza, wamekubaliana na wameandika kumbukumbu. Lakini hakuna anayejua nani anapaswa kufanya nini na lini. Ndiyo maana kikao kingine kinaanza kwa kuuliza: "Hili tulilokubaliana mara iliyopita limefikia wapi?"

Kila kikao kinapaswa kuishia kwenye mambo matatu: nini kifanyike, nani akifanye na kikamilike lini. Wataalamu wanashauri kila mshiriki anayebeba jukumu aseme wazi anachokwenda kutekeleza na muda wa kukamilisha, kisha makubaliano hayo yaandikwe na kusambazwa.

Mwisho, kikao kizuri si kile kilichokuwa na majadiliano mengi. Kikao kizuri ni kile ambacho watu walijua kwa nini wamekutana, walijadili jambo muhimu, wakafanya uamuzi na wakaondoka wakijua hatua inayofuata.

Kama hakuna uamuzi, hatua au matokeo yanayotarajiwa, wakati mwingine uamuzi bora zaidi ni kutokuitisha kikao kabisa.

NA JUNAYNAT ALLY DAMA
0789 201 383

Malezi rika kwa rika

SEHEMU YA 5

Miaka 13-18: Kijana wako hahitaji polisi tu– anahitaji mzazi anayeweza kuzungumza naye

MTOTO anapoingia ujana, wazazi wengi huanza kuwa na hofu. Marafiki wanapata nafasi kubwa, simu na mitandao vinakuwa sehemu ya maisha yake, anataka faragha, ana maoni yake na wakati mwingine anaweza kuonekana kupinga kila jambo.

Lakini miaka 13 hadi 18 si kipindi cha kuacha malezi. Ni kipindi cha kubadili namna ya kulea.

Katika umri huu kijana anajenga utambulisho wake. Anaanza kujiuliza: Mimi ni nani? Ninaamini nini? Nitataka kufanya kazi gani? Marafiki wa aina gani ninaowataka? Nataka kuwa mtu wa aina gani?

Kadiri anavyokua, uwezo wake wa kufikiri, kuchambua mambo na kueleza sababu za maamuzi yake huongezeka. Wakati huohuo, bado anaweza kuathiriwa na marafiki, hisia na mazingira. Ndiyo maana anahitaji nafasi zaidi ya kufanya maamuzi, lakini bado anahitaji mwongozo wa wazazi.

Kwa hiyo, usimamizi wa kila hatua unapaswa kupungua hatua kwa hatua na nafasi yake ichukuliwe na mazungumzo, mipaka iliyo wazi na uwajibikaji.

Kijana akisema, “Sikubaliani,” usione moja kwa moja kwamba amekuwa mkorofi. Sikiliza anachosema. Haimaanishi lazima ukubaliane naye. Lakini anahitaji kujifunza kueleza hoja, kusikiliza hoja nyingine na kukubali kwamba wakati mwingine mzazi atasema hapana.

Hapa ndipo uhusiano unapokuwa muhimu kuliko wingi wa amri. Usimuulize maswali kana kwamba unamhoji polisi. Mazungumzo madogo yanaweza kufungua mlango wa jambo kubwa.

Na unapozungumza naye, weka simu pembeni. Kijana anatambua haraka tofauti kati ya mzazi aliyepo chumbani na mzazi anayemsikiliza kweli.

Ujana pia huleta mabadiliko ya mwili na hisia. Kuna masuala ya mwonekano, urafiki, shinikizo la marafiki, mahusiano na jinsia. Usisubiri TikTok, marafiki au mitandao iwe walimu wa kwanza.

Zungumza naye kwa lugha inayolingana na umri kuhusu mwili unaobadilika, mahusiano yenye afya yanayozingatia mipaka ya Allah, ridhaa, usalama na namna ya kutoka katika hali inayomweka katika hatari. Kijana akiuliza swali nyeti, usikimbilie kufikiri kwamba lazima tayari analifanya jambo analoulizia.

Simu nayo haiwezi kutengwa na malezi ya sasa.

Wekeni makubaliano kuhusu muda wa matumizi, faragha, picha binafsi, watu anaowasiliana nao na maudhui anayoyatumia. Mfundishe kuwa kitu anachoweka mtandaoni kinaweza kuhifadhiwa au kusambazwa.

Lakini uangalizi usigeuke upelelezi wa kila dakika. Heshimu faragha yake huku ukijua kinachoendelea. Pale panapokuwa na dalili za ulaghai, unyanyasaji, dawa za kulevya, kujiumiza au hatari nyingine, mzazi ana wajibu wa kuingilia kati.

Kadiri anavyokaribia utu uzima, mpe majukumu halisi. Ajifunze kupanga muda, kusimamia fedha, kufanya kazi za nyumbani, kujiwekea malengo, kupanga masomo na kufikiria kazi au taaluma ya baadaye.

Uhuru uongezeke pamoja na uwajibikaji.

Akifanya kosa lisiloleta hatari kubwa, usikimbilie kumwondolea kila nafasi ya kufanya uamuzi. Wakati mwingine matokeo ya uchaguzi wake yanaweza kumfundisha zaidi kuliko hotuba ndefu.

Pia, chagua mambo ya kupigania. Si kila chumba kisichopangwa, mavazi au maoni tofauti yanahitaji vita kubwa. Linda mambo ya msingi: usalama, afya, elimu, heshima, maadili na tabia.

Usipuuze mabadiliko makubwa yanayodumu katika usingizi, ulaji, masomo, kujitenga, hasira kali au kupoteza kabisa hamu ya mambo aliyokuwa akiyafurahia. Haya yanaweza kuwa ishara kwamba kijana anahitaji msaada zaidi, na wakati mwingine ushauri wa kitaalamu.

Kwa familia ya Kiislamu, malezi hayo yana tabaka jingine muhimu: kijana anapoingia baleghe, anaanza pia kuwajibika mwenyewe katika ibada na matendo yake. Hivyo, lengo si tu kumfanya akufuate wewe, bali kumsaidia ajenge uhusiano wake mwenyewe na Allah.

Mfundishe swala, Qur’an na maadili kwa maelezo na mfano wako. Akiuliza, “Kwa nini dini inakataza hili?” usione swali kuwa uasi. Ni bora aje na shaka yake kwako kuliko aitafutie jibu kwa chanzo kisichoaminika.

Qur’an inasisitiza upole na mashauriano katika kuwaongoza wengine [Qur’an, 3:159]. Katika malezi pia, upole hauondoi mipaka; unafanya ujumbe uwe rahisi kupokelewa.

Na kijana asimjue Allah kupitia hofu ya adhabu pekee. Ajifunze pia kumtambua kama Mwenye rehema, Mwenye kusikia dua na Mwenye kutegemewa katika shida. Utafiti unaounganisha mtoto anayejisikia salama katika uhusiano na wazazi wake ana msingi mzuri zaidi katika mahusiano mengine; ikiwemo katika kujenga ukaribu na Allah.

Mzazi naye awe mfano. Ukimtaka awe mwaminifu, usidanganye mbele yake. Ukimtaka adhibiti hasira, akuone ukiomba msamaha unapokosea. Ukimtaka awe na uhusiano na Allah, fanya dua pamoja naye, si kwa ajili yake tu.

Hatimaye, kijana wako hahitaji mzazi anayesubiri kosa ili aadhibu. Anahitaji mwongozo, mipaka na mtu anayemwamini. Baki kuwa mahali salama anapoweza kurudi.

Kwa sababu katika miaka hii, ushawishi mkubwa wa mzazi haujengwi na wingi wa amri—unajengwa na uhusiano unaomfanya kijana bado atake kuja kuzungumza nawe.

Na Samrath Msuya
0789 201 383

Ubunifu katika ufundishaji hisabati

SEHEMU YA MWISHO

4

Darasa la hesabu linaweza kuwa na uhai: Mwalimu aanzie wapi?

Baada ya kuona kwamba hesabu si kukariri kanuni pekee, na kwamba ipo katika maisha yetu ya kila siku, swali linalofuata ni la vitendo: Mwalimu anaweza kufanya nini ili mwanafunzi afikiri zaidi na asiishie kufuata maelekezo?
Jibu halihitaji mapinduzi makubwa darasani. Wala si lazima shule iwe na kompyuta, skrini kubwa au vifaa vya gharama. Mabadiliko yanaweza kuanza na namna mwalimu anavyouliza maswali, anavyopokea majibu na anavyowapa wanafunzi nafasi ya kufikiri.

Uliza zaidi ya "jibu ni nini?"

Katika kipindi cha kawaida cha hesabu, mara nyingi lengo huwa kupata jibu sahihi. Lakini mwalimu anaweza kuongeza maswali madogo: "Umefikaje hapo?" "Kwa nini umechagua njia hiyo?" "Kuna njia nyingine?"

Maswali hayo yanamlazimisha mwanafunzi kueleza fikra zake. Pia yanamsaidia mwalimu kujua kama mwanafunzi ameelewa au amekariri tu hatua alizooneshwa.

Maswali yanayowapa wanafunzi nafasi ya kutoa mawazo yao yanaweza kuendeleza uwezo wao wa kufikiri kwa kujitegemea na kujifunza kutokana na mitazamo tofauti.

Ruhusu njia tofauti

Si kila swali la hesabu linapaswa kuishia na wanafunzi wote kutumia njia moja.

Mara nyingine, baada ya kupata jibu, mwalimu anaweza kuuliza: "Nani amefanya kwa njia tofauti?" Kisha darasa likalinganishe njia hizo.

Hapo mwanafunzi anaanza kuona kwamba hesabu si kuiga tu alichofanya mwalimu. Anaweza kutumia maarifa aliyonayo kufikia jibu kwa njia nyingine, mradi njia hiyo ina mantiki.

Tafiti kuhusu ubunifu katika hesabu zinaonesha kuwa nafasi ya kutafuta njia mbalimbali inaweza kukuza uwezo wa mwanafunzi wa kutoa mawazo mengi, kubadili mkakati na kutafuta suluhisho tofauti.

Usiogope mwanafunzi kukosea

Darasa ambalo mwanafunzi anaogopa kutoa jibu lisilo sahihi linaweza kuwa darasa la ukimya. Lakini kosa linaweza kuwa sehemu ya somo. Badala ya kusema tu "umekosea", mwalimu anaweza kuuliza mwanafunzi alifikiria nini na ni sehemu gani ingeweza kubadilishwa.

Hapo watoto wengine pia hujifunza. Wanaona kwamba kukosea si mwisho wa kujifunza, bali kunaweza kuwa mwanzo wa kuelewa jambo vizuri zaidi. Mazingira yanayoruhusu kujaribu, kujadili na kurekebisha mawazo yana nafasi muhimu katika kujenga ubunifu na ushiriki wa wanafunzi katika hesabu.

Wape muda wa kufikiri

Mwalimu akiuliza swali na kutaka jibu papo hapo, mara nyingi wanafunzi wale wale wenye kasi ndiyo watajibu.

Wengine wanaweza kuelewa, lakini wanahitaji muda kidogo zaidi. Hivyo, wakati mwingine ni vizuri kuuliza swali na kuwapa wanafunzi muda wa kufikiri kabla ya kuchagua wa kujibu.

Kasi si sawa na uwezo wa kufikiri.

Utafiti kuhusu ubunifu katika utatuzi wa matatizo unaonesha kuwa wanafunzi wanahitaji muda wa kuchunguza, kujaribu, kukwama na kubadili njia. Mchakato huo wenyewe ni sehemu ya kujifunza.

Waruhusu wanafunzi kuuliza

Kwa kawaida, mwalimu huuliza na mwanafunzi hujibu. Lakini wakati mwingine mpangilio huo unaweza kubadilishwa.

Mwalimu anaweza kuonesha picha, takwimu, umbo au hali fulani na kuuliza: "Ni maswali gani ya hesabu tunaweza kuuliza kuhusu hiki?"

Wanafunzi wanapotunga maswali yao wenyewe, wanaanza kuona jambo ambalo hawakuzoea: hesabu si kutafuta majibu tu. Ni pia kutambua jambo linalohitaji kuchunguzwa.

Njia ya kuwafanya wanafunzi watunge matatizo au maswali yao imehusishwa na kukuza uwezo wa kutatua matatizo, kuelewa dhana na kufikiri kwa ubunifu.

Tumia mazingira yaliyopo

Ubunifu katika kufundisha hauhitaji vifaa vya gharama kubwa.

Darasa, uwanja wa shule, saa, kalenda, fedha, vipimo, chupa, maumbo, michezo na mazingira yanayoizunguka shule vinaweza kutoa fursa za kuzungumzia hesabu.

Muhimu ni kumsaidia mwanafunzi kuona uhusiano kati ya kile kilicho kwenye kitabu na kile anachokiona katika maisha.

Hata sanaa, muziki na uandishi vinaweza kusaidia. Mwanafunzi anaweza kuchora anachofikiria, kueleza kwa maneno namna alivyotatua tatizo au kutunga tatizo lake mwenyewe.

Mwalimu awe mwongoza fikra

Mbinu hizi hazipunguzi umuhimu wa mwalimu. Kinyume chake, zinahitaji mwalimu mwenye uwezo wa kujua wakati gani aeleze na wakati gani awaache wanafunzi watafute. Mwalimu si lazima awe chanzo cha kila jibu. Wakati mwingine kazi yake kubwa ni kuuliza swali linalomfanya mwanafunzi afikiri zaidi.

Ijulikane kuwa, walimu wana nafasi muhimu katika kujenga mazingira ambayo mawazo tofauti, uchunguzi na ubunifu vinathaminiwa.

Anza na jambo moja

Hakuna haja ya mwalimu kubadilisha kila kitu kwa siku moja.

Anaweza kuanza na jambo moja katika kipindi chake kijacho. Badala ya kuuliza "Jibu ni nini?", aulize pia, "Umefikaje hapo?" Badala ya kuonesha njia pekee, awaulize kama kuna njia nyingine. Badala ya kumkatisha aliyekosea, amsaidie kueleza alichofikiria.

Mabadiliko hayo yanaonekana madogo. Lakini yanaweza kuanza kubadilisha darasa kutoka mahali pa kufuata hatua na kuwa mahali pa kufikiri, kujaribu na kugundua.

Na huenda hapo ndipo mtoto anapoanza kugundua jambo muhimu: hesabu si somo la kuogopa. Ni somo analoweza kulifikiria, kulijaribu na kulielewa.

Na Junaynat Ally Dama

Uandishi wa habari kwa msaada wa AI

SEHEMU YA 4

AI katika takwimu, nyaraka na uchunguzi wa habari

Mwandishi anaweza kukabidhiwa ripoti ya kurasa 300, bajeti yenye majedwali mengi au taarifa ya ukaguzi iliyojaa takwimu. Ndani yake huenda kukawa na habari muhimu, lakini changamoto ya kwanza huwa ni kujua pa kuanzia.

Hapa akili bandia (AI) inaweza kuwa msaada mkubwa. Inaweza kusaidia kupitia nyaraka nyingi, kupanga taarifa na kubaini maeneo yanayostahili kuchunguzwa zaidi. Lakini kanuni yake ni ile ile: AI inaweza kukuonesha pa kuchimba; haiwezi kuwa ushahidi wa kile kilichopo chini.

Ripoti ndefu isiwe kikwazo

Fikiria mwandishi ana ripoti kubwa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Kusoma ripoti hiyo kwa makini bado ni muhimu, lakini AI inaweza kumsaidia kupata picha ya awali ya yaliyomo.

Anaweza, kwa mfano, kuiomba itambue maeneo yanayozungumzia matumizi makubwa, ongezeko au upungufu wa fedha, miradi iliyochelewa au hoja zinazojirudia. Anaweza pia kuitumia kupanga masuala yanayofanana ili ajue sehemu gani anapaswa kuisoma kwa undani zaidi.

Hilo linaweza kuokoa muda. Badala ya kuanza bila kujua pa kuelekea, mwandishi anapata maeneo yanayoweza kuwa na jambo la kufuatilia. Lakini muhtasari wa AI haupaswi kuchukuliwa moja kwa moja na kuchapishwa. Mwandishi lazima arudi kwenye ukurasa husika wa ripoti na kuthibitisha kilichoandikwa.

Takwimu zinaweza kuficha habari

Wakati mwingine habari haipo katika sentensi, bali katika namba. Takwimu za miaka kadhaa zinaweza kuonesha kuwa gharama zimeongezeka kwa kasi, eneo moja limefanya tofauti kubwa na mengine au kiasi kilichotengwa hakilingani na kilichotumika.

Majedwali makubwa yanaweza kuwa magumu kuyachunguza kwa macho, hasa mwandishi akiwa na muda mdogo. AI inaweza kusaidia kupanga takwimu, kulinganisha vipindi na kutambua mabadiliko makubwa yanayostahili kuuliziwa.

Kwa mfano, mwandishi anaweza kuiomba ichunguze takwimu za matumizi ya taasisi kwa miaka kadhaa na itambue maeneo yenye ongezeko au upungufu mkubwa. Jibu hilo halitakuwa mwisho wa habari, bali mwanzo wa maswali mapya.

Tofauti si lazima iwe ufisadi

Hili ni muhimu sana katika habari za uchunguzi. AI ikibaini kwamba matumizi fulani yameongezeka mara mbili, hilo halimaanishi moja kwa moja kwamba kuna ubadhirifu au ufisadi. Huenda bajeti iliongezeka, mradi ukapanuka, bei zikabadilika au mfumo wa kuhesabu ukabadilishwa. Hivyo, jambo lisilo la kawaida ni mwanzo wa swali, si mwisho wa uchunguzi.

Mwandishi anatakiwa kuendelea kuuliza: Kwa nini takwimu zimebadilika? Ripoti yenyewe inaeleza nini? Taasisi husika inasemaje? Kuna nyaraka nyingine zinazoweza kuthibitisha au kueleza tofauti hiyo?

Hapo ndipo AI inapokoma na kazi halisi ya uandishi wa habari inaanza.

Linganisha nyaraka kwa haraka

Mwandishi anaweza pia kuwa na matoleo mawili ya waraka, bajeti za miaka tofauti au taarifa mbili zinazozungumzia jambo moja. AI inaweza kusaidia kutambua kilichoongezwa, kilichoondolewa au kilichobadilishwa.

Inaweza pia kusaidia kuona takwimu ambazo hazifanani au kauli zilizobadilika kutoka waraka mmoja kwenda mwingine. Hii inaweza kuwa muhimu katika kufuatilia sera, bajeti, mikataba au taarifa za taasisi.

Lakini hata hapa, mwandishi anapaswa kurudi kwenye nyaraka halisi. Mfumo unaweza kukosa mstari, kuchanganya jedwali au kutafsiri vibaya lugha ya kitaalamu.

Muulize AI kwa malengo mahsusi

Badala ya kusema, "Niambie habari iliyopo kwenye ripoti hii," ni bora mwandishi aulize maswali mahsusi. Anaweza kutaka kujua maeneo yenye mabadiliko makubwa ya matumizi, hoja zinazojirudia, takwimu zinazotofautiana na miaka iliyopita au maswali ambayo anapaswa kuwauliza wahusika.

Hapo AI inakuwa chombo cha kusaidia uchunguzi, si mhariri anayemchagulia mwandishi habari.

Unaweza kusema: "Nina ripoti hii ya bajeti. Nisaidie kutambua maeneo yenye mabadiliko makubwa ya matumizi, takwimu zinazohitaji maelezo zaidi na maswali ambayo mwandishi anaweza kuuliza. Usihitimishe kuwa kuna kosa au ubadhirifu bila ushahidi."

Kwa nyaraka nyeti, hasa mikataba, taarifa za siri au nyaraka ambazo hazijachapishwa, mwandishi anapaswa kuwa makini sana kabla ya kuzipakia kwenye mfumo wa AI. Masuala ya faragha na ulinzi wa taarifa tutayajadili kwa kina katika makala nyingine.

Muhimu tulichojifunza, AI inaweza kubaini jambo lisilo la kawaida. Mwandishi ndiye anayepaswa kuthibitisha kama kweli kuna habari.

ربيع ثان

MAKALA YA AFYA

Na Junaynat Ally Dama

Kiharusi kinawafikia vijana zaidi, utafiti waonya

Kwa muda mrefu kiharusi kimeonekana zaidi kama ugonjwa wa wazee. Lakini utafiti mpya unaonyesha kwamba vijana nao hawapaswi kuipuuzia afya ya moyo, mishipa na ubongo.

Utafiti uliochapishwa mtandaoni Septemba 23, 2026 katika jarida la kitabibu Neurology umebaini kuwa kiwango cha kiharusi miongoni mwa watu wenye umri wa miaka 20 hadi 54 kilikaribia kuongezeka mara mbili katika kipindi cha karibu miaka 30. Utafiti huo uliochapishwa katika jarida la Neurology uliandaliwa na timu ya watafiti 29, wakiongozwa na Emily R. Fisher na wenzake. Umeorodheshwa kuchapishwa katika toleo la Neurology la Oktoba 27, 2026.

CNN, iliyoripoti matokeo hayo Septemba 23, imeeleza kuwa wataalamu wanaona mwenendo huo kuwa muhimu kwa sababu kiharusi kinapotokea katika umri mdogo kinaweza kumuacha mtu na ulemavu wakati bado anafanya kazi, analea watoto na kutekeleza majukumu mengine ya maisha.

Kiharusi kwa vijana karibu mara mbili

Watafiti walichunguza visa vya kiharusi vilivyolazwa hospitalini katika kaunti tano za eneo la Cincinnati na Northern Kentucky nchini Marekani. Walitumia vipindi sita vya utafiti: 1993–1994, 1999, 2005, 2010, 2015 na 2020. Visa vilihakikiwa na madaktari waliobobea katika kiharusi.

Kwa jumla walibaini visa 2,076 vya watu wenye miaka 20–54 waliopata kiharusi kwa mara ya kwanza. Kiwango cha kiharusi kilipanda kutoka visa 33.9 kwa watu 100,000 mwaka 1993–1994 hadi 62.18 mwaka 2020.

Kinachovutia zaidi ni kwamba katika kipindi hicho hicho, kiwango kwa watu wenye umri mkubwa kilishuka kutoka visa 618.78 hadi 453.04 kwa watu 100,000.

Hivyo, wakati maendeleo katika kinga na tiba yanaonekana kwenda sambamba na kupungua kwa kiharusi kwa wazee katika jamii hiyo, vijana walikuwa wakisogea upande tofauti.

Kuziba kwa mshipa kuliongoza ongezeko

Ongezeko kubwa lilitokana na aina ya kiharusi inayotokea pale damu inaposhindwa kufika sehemu ya ubongo kwa sababu mshipa umeziba. Kiwango cha aina hii kilikaribia mara mbili, kutoka visa 23.8 kwa watu 100,000 mwaka 1993–1994 hadi 47.3 mwaka 2020.

Watafiti pia waliona kuongezeka kwa baadhi ya vihatarishi miongoni mwa waliopata kiharusi.

Shinikizo la juu la damu liliongezeka kutoka asilimia 47 hadi 60; kisukari kutoka asilimia 19 hadi 26; na mpapatiko usio wa kawaida wa moyo kutoka asilimia moja hadi sita. Matumizi ya baadhi ya vilevi nayo yaliongezeka kutoka asilimia tano hadi 40, sehemu kubwa ikihusishwa na ongezeko la matumizi ya bangi.

Hata hivyo, watafiti wanaonya dhidi ya kuhitimisha kwamba vihatarishi hivyo ndivyo vilisababisha ongezeko lote. Utafiti haukuwa na kundi linganishi la watu ambao hawakupata kiharusi, hivyo hauwezi kuthibitisha uhusiano wa moja kwa moja wa kisababishi.

Dkt. Robinson anasema unene kupita kiasi, kiwango kikubwa cha lehemu katika damu na maisha ya kutofanya shughuli za mwili vinaweza pia kuchangia. Huenda, kwa hiyo, hakuna sababu moja bali mchanganyiko wa mambo kadhaa.

Habari njema: vifo vimepungua kidogo

Pamoja na kuongezeka kwa visa, utafiti ulibaini kupungua kwa kiwango cha vifo ndani ya siku 30 baada ya kiharusi miongoni mwa vijana: kutoka asilimia 11.7 mwaka 1993–1994 hadi asilimia 9.4 mwaka 2020.

Kupungua huko kulionekana zaidi kwa aina za kiharusi zinazohusisha kuvuja damu ndani au kuzunguka ubongo.

Hii inaweza kumaanisha vijana wengi zaidi wanaonusurika, lakini pia ina maana baadhi yao wanaweza kuishi kwa muda mrefu na athari za kiharusi.

Vijana wafanye nini?

American Heart Association inapendekeza kula vizuri, kufanya mazoezi, kuepuka tumbaku, kupata usingizi wa kutosha na kudhibiti uzito, shinikizo la damu, sukari na lehemu. Dkt. Robinson anashauri vijana pia kufanya uchunguzi wa afya badala ya kusubiri mpaka waone dalili.

Dkt. Michelle Leppert wa Tufts Medical Center anakumbusha kuwa kiharusi bado si tukio la kawaida kwa vijana, hivyo hakuna sababu ya kuingiwa na hofu. Lakini kupima afya mara kwa mara kunaweza kusaidia kubaini vihatarishi mapema.

Takwimu hizi ni za jamii maalumu nchini Marekani, si Tanzania, hivyo haziwezi kuhamishwa moja kwa moja kwetu. Lakini ujumbe wake ni muhimu popote: ujana si kinga dhidi

UKHTI FATIMA SS

Kuna Qadar, jifunze kutojibebesha kila lawama

Kuna watu ambao jambo linapoharibika, swali lao la kwanza si "Nini kimetokea?" bali "Nimekosea wapi?" Ndoa ikivunjika, anajilaumu. Mtoto akifeli, anajilaumu. Rafiki akikasirika, anatafuta kosa lake. Kazi ikiharibika hata kutokana na mazingira ambayo hakuwa na uwezo wa kuyadhibiti, bado anasema: "Laiti ningefanya hivi..."

Kukubali kosa ni tabia njema. Lakini kuwajibika na kujilaumu si kitu kimoja. Uwajibikaji unasema: "Hapa nilikosea. Nitajifunza na kurekebisha." Kujilaumu kupita kiasi husema: "Kila kitu kimeharibika kwa sababu yangu. Mimi ndiye tatizo."

Hapo ndipo saikolojia inaanza kuona hatari.

Makala ya iliyochapishwa katika tovuti ya Psychology Today ya Septemba 22, 2026, inaeleza kuwa lawama zinaweza kuwa na kazi muhimu. Mtu aliyekosea anapokubali kosa, anaweza kuomba msamaha, kurekebisha madhara na kujenga upya uaminifu. Tatizo huanza tunapojibebesha lawama hata kwa mambo ambayo hatukuwa na uwezo wa kuyazuia.

Wakati mwingine kujilaumu ni njia ya akili kutafuta udhibiti katika mazingira ambayo kwa kweli hatuna udhibiti.

Kwa Muislamu, hapa ndipo dhana ya Qadar inapoweza kutoa mizani muhimu ya kisaikolojia na kiroho. Imani ya Qadar haitufundishi kutowajibika kwa makosa yetu, bali kutambua kuwa si kila kinachotokea duniani kiko ndani ya uwezo wetu. Mwanadamu ana jukumu la kufanya uchaguzi, kuchukua tahadhari na kuwajibika kwa alichofanya, lakini pia anakubali kuwa matokeo yote hayako mikononi mwake.

Fikiria mtu aliyepata ajali. Anaweza kurudia kichwani: "Laiti nisingetoka nyumbani dakika hiyo," au "Laiti ningepitia barabara nyingine."

Kauli hizo zinaweza kumpa hisia kwamba angeweza kuzuia kilichotokea. Ukweli mgumu zaidi ni kukubali kwamba baadhi ya mambo mabaya hutokea licha ya juhudi zetu.

Hapa ndipo kujilaumu kunaweza kugeuka kuwa mapambano yasiyoisha dhidi ya Qadar. Akili inaanza kujenga dunia ya "laiti": laiti nisingekwenda, laiti ningesema hivi, laiti ningefika dakika tano mapema.

Kujifunza kutokana na uamuzi mbaya ni muhimu, lakini kuishi maisha yote ukijaribu kuandika upya jambo ambalo tayari limetokea kunaweza kukuongezea maumivu bila kubadilisha yaliyopita.

Kwa namna hiyo, kujilaumu kunaweza kutupa hisia bandia ya udhibiti.

Hali hii inaweza kuanzia utotoni.

Watoto wanapokulia katika familia zenye migogoro, talaka, mzazi mwenye hasira au matatizo mengine, wanaweza kujiona wao ndio chanzo. Mtoto anaweza kufikiri: "Kama ningekuwa mtoto mzuri zaidi, baba na mama wasingegombana."

Kitaalamu, mtoto bado hana uwezo mpana wa kuelewa sababu changamano za matatizo ya watu wazima. Kujilaumu kunaweza kuwa njia rahisi ya kuifanya dunia ionekane inaeleweka: "Kama kosa ni langu, basi labda nikibadilika mambo yatakuwa sawa."

Tatizo ni kwamba mtoto anaweza kuingia utu uzima akiwa bado amebeba kanuni hiyo. Anaanza kuomba msamaha hata pale ambapo hajakosea. Anajitahidi kupita kiasi kuwafurahisha watu. Anaogopa migogoro. Anaona ni jukumu lake kuhakikisha kila mtu yuko sawa.

Kujilaumu kwa muda mrefu kunaweza kwenda sambamba na huzuni, wasiwasi, aibu, kujiona huna thamani na kujikosoa kupita kiasi. Katika watu waliopitia matukio ya kutisha, kunaweza pia kuhusishwa na dalili za msongo baada ya kiwewe.

Lakini mtu anawezaje kujinasua?

Hatua ya kwanza ni kuikamata fikra kabla haijawa hukumu. Unapojisikia kusema "Ni kosa langu," jiulize: Ushahidi ni upi? Ni mambo gani mengine yalichangia? Ni sehemu gani kweli ilikuwa ndani ya uwezo wangu?

Mbinu moja inayotumiwa katika tiba ya kisaikolojia ni kuandika sababu zote zilizochangia tukio na kugawanya uwajibikaji kwa uhalisia. Mara nyingi tunapofanya hivyo, tunagundua tulikuwa tumebeba asilimia 100 ya lawama kwa jambo ambalo lilikuwa na sababu nyingi.

Swali jingine lenye nguvu ni hili: Kama rafiki yangu angepitia jambo hili, ningemlaumu kwa ukali ninaojilaumu mimi? Kama jibu ni hapana, huenda tatizo si kosa lako pekee bali namna unavyojitazama.

Pia, badala ya kuuliza bila mwisho, "Ni kosa langu?", jaribu kuuliza: "Ninaweza kufanya nini sasa?" Kama ulikosea, omba msamaha. Rekebisha unachoweza. Jifunze. Kama jambo halikuwa ndani ya uwezo wako, jifunze kuliacha.

Chanzo kimoja kimetumia mfano mzuri: kujilaumu ni kama kiti cha kubembea—unaendelea kusogea, lakini hufiki popote. Uwajibikaji ni kutembea; unaweza kuchoka, lakini unasonga mbele. Kwa hiyo, Qadar na uwajibikaji si maadui.

Unaweza kusema: "Nilifanya nilichoweza. Hapa nilikosea na nitarekebisha. Lakini sehemu hii haikuwa mikononi mwangu." Huo si uzembe wala kujifariji kwa uongo. Ni kukubali mipaka ya uwezo wa mwanadamu.

Kisaikolojia, kukubali mipaka hiyo kunaweza kumsaidia mtu kuacha kujitesa kwa mambo ambayo hawezi kuyabadilisha. Hatimaye, uponyaji hauhitaji mtu kujitangaza kuwa hana makosa. Unahitaji uwezo wa kutofautisha kati ya kosa nililofanya na mimi nilivyo.

Ulikosea? Rekebisha. Hukuweza kudhibiti kilichotokea? Kubali mipaka yako.

Kujifunza kutokana na kosa ni hekima. Kuwajibika ni wajibu. Lakini kujilaumu kwa kila kilichotokea ni kujibebesha mzigo ambao wakati mwingine ni wa Qadar, si wa makosa yako.